

MASWALI NA MAJIBU

 ...Ndugu zanguni, nime-...nadhani kulikuwa na yaliyosalia ambayo sikuyafikia; singeendelea tena. Lo, nilichoshwa sana na maono. Ona? Na yamenikulia mengi, yapata kumi na matano au ishirini adhuhuri ya leo, na hayo yanidhoofisha mno. Nikigusia tu hapa na pale. Nilitoka nje; nilisema, “Ndugu Neville, kama—kama unaweza kuendelea, endelea; nataka kuponyoka niende nyumbani.” Nilisema, “Niko karibu tu kuanguka, hata moyo wangu unadunda-dunda na kurukaruka.” Nami nilisema, “Mi—mimi—ni vigumu kwangu kusimama tena.”

² Yeye alisema, “Ndugu Branham, watu wamekuwa wakiniuliza mimi kama ungemaliza kuyajibu maswali hayo.” Na mi—mi—mimi sitaki kuepa wajibu wangu kamwe. Namthamini Ndugu Neville. Na labda kwa dakika chache nitafanya kadiri niwezavyo. Nami ni—ninajua kuna...Billy alipoingia mle; nilisema, “Uliwapata wote?”

³ Yeye akasema, “Baba, kuna ishirini au zaidi waliobakia—wangali wanangojea.” Kwa hivyo singepata...Hao ni watu wanaozidi thelathini, na karibu maono ishirini na matano; kwa hivyo unaweza kuwaza wapi ninakosimama. Kwa hivyo ni—nimechoka sana, nimechoka sana akili. Lakini tutaomba, tuanzie moja kwa moja mahali tulipoachia maswali haya. Halafu, ni—nitakapoenda Arizona haya yakiwa niani mwangu, nitasumbuliwa wakati wote. Nitarudi hivi punde, Bwana akipenda, na nihubiri juu ya jambo hilo upesi iwezekanavyo, juu ya usahihi wa ndoa na talaka. Na tuombe.

⁴ Mungu mpendwa, Wewe wajua moyo wangu, na Wewe wajua ninavyojisikia; unajua yote kunihusu. Nami naomba, Mungu; kuna watu wengi. . . Ninawaacha waendeleo kungoja kwa muda mrefu sana, Bwana; ni wengi sana. Lakini ninashukuru sana kwamba siamini kulikuwa na mmoja aliyeingia leo ila yule aliyesaidiwa. Naamini kila mmoja wao aliondoka amefurahi na ameridhika. Mambo ambayo singeyajibu mimi mwenyewe, Wewe ulishuka kwa maono na kuyafunua nyuma katika maisha yao (wameketi hapa, wengi wao, hivi sasa wakiyasikia na wanajua ni kweli,) na ukawafunuliwa mambo yaliyokuwa kule nyuma maishani mwao ambayo yalisababisha mambo hayo kutukia, wao wanajua, Bwana. Haiwezekani kamwe kwangu kujua hayo pasipo msaada Wako.

⁵ Nami naomba, Baba wa Mbinguni, kuwa ijapokuwa nimechoka, lakini nina furaha kuwa mtumishi Wako. Nami naomba kuwa utawabariki wale waliokuwa wakingoja, wengi wao waliotaka kuingia. Nami ni—ni—ninatumainia, Mungu,

kuwa wata—watashughulikiwa, Roho Mtakatifu Wako mkuu atawapa wao cho chote wanachohitaji.

⁶ Nisaidie kumaliza maswali haya, Mungu mpendwa, au kufanya vizuri niwezavyo nayo, kusudi watu Wako wajibiwe maswali yao. Niliwauliza wayaandike. Waliyaandika nami najisikia nina wajibu wa kujaribu kuyajibu kwa ajili yao. Kwa hivyo naomba kuwa utanipa nguvu ili niweze kufanya wajibu wangu Kwako na kwa watu hawa. Katika Jina la Yesu naomba. Amina.

⁷ Sasa, tutaaanzia papa hapa ambapo tuliachia asubuhi hii. Baadhi ya haya huenda nisiweze kusoma, kwa sababu kwamba—nimepwewa kidogo na sauti, kwa sababu nimekuwa nikiongea sana. Wangapi walikuwa kwenye upambanuzi leo ambao walifurahia sana Mungu kuwapeni ninyi yale...? Ona? Hizo ndizo bora ya zote, ni ibada za namna hiyo. Mambo unayotaka kujua na mambo ambayo yameisha fichwa maishani yanafunuliwa na kueleza.

⁸ Na—na kumbuka, mengi ya mambo haya...Sasa, wengi wenu mnajua bila shaka kuna mambo ya kufadhaisha yaliyosemwa na kufichuliwa, lakini hakuna ye yote ajuaye hayo ila mimi na Mungu. Na yale mliyoambiwa, hayo yapaswa yawe kati yenu na Mungu; yaacheni tu. Na... Wangapi wenu mnajua kuwa Bwana alifunua mambo haya yalivyokuwa yalifanywa ili kuwasaidia. Inueni mikono yenu kama yaliwasaidia. Ona? Bila hata kujua hao watu, hakuna lo lote kuwahusu, ila Yeye—Yeye alilifanya.

⁹ Sasa, hebu tuyaendee maswali upesi tuwezavyo sasa tuone kama tunaweza kupata...Kuna lingine pia ambalo liko hapa mahali fulani. Linasema, “Nambari tatu.” Naamini ni barua; naam, ni barua tu. Nasikitika. Nitaziweka juu hapa ninapozifikia, nami nafikiri...Naam, bwana, hii pia ni barua. Nayo inasema, “Swali,” lakini naamini ni barua, swali katika barua. La, sivyo, ni swali kuhusu ndoto. Vema, nitasoma hiyo ndoto kisha nitaona kama Bwana atanipa tafsiri yake, na kukueleza wewe jinsi tu niwezavyo. Nadhani umeandika anwani yako. Hebu tuone kama ipo; kama haipo, nitakusihi uandike anwani yako, mtu yule aliye na swali hili na—na ndoto. La, hukuandika.

¹⁰ Ye yote aliyeandika barua hii (ina—nimeandikiwa tu), mpe Billy anwani yako, ili nikishika njia kuelekea Arizona, nitaenda jangwani na kuomba. Na kama Yeye atanipa tafsiri yake, nitajua nikiandika nitaituma wapi (mwaona? Bila hilo pale kutoa tafi—) Yeye akinipa. Lakini sitasema isipokuwa itolewe, kwa sababu naweza tu kufanya hivyo; ndipo najua nitakuwa sahihi. Sasa.

376. Je, Bibi-arusi, wale wanaouamini Ujumbe huu, wataenda magharibi, je, hatimaye watakutania kule, nakusudia?

377. Na ni (Sasa, ngoja kidogo hili ni...leta...Hebu kwa kidogo tu. Ee! La, sivyo, lina "R-e-v." Nilidhani ni sura ya Revelation (Ufunuo), na inaonekana kama "Rev. Capps." na ni—ni—nilitatanishwa kidogo nalo. Ni...Kama ukitazama, bila shaka inaonekana hivyo. Ona? Lilikuwa "Rev. (Kasisi) Capps." kisha likaendelea hapa...La, ni sahihi.) **Je, Ufunuo sura ya 12, inanena habari za Bibi-arusi?**

¹¹ La! "Sasa, je, hatimaye Bibi-arusi ataenda magharibi, hatimaye?" Sivyo kadiri nijuavyo; Bibi-arusi yuko ulimwenguni kote, duniani mwote. Sasa, kila mtu anayefahamu hilo aseme, "Amina!" [Kusanyiko linaitikia, "Amina! —Mh.]

Haidhuru uko wapi, unakufia wapi, lo lote lile, ukifa katika Kristo, Mungu atakuleta pamoja Naye. Haidhuru kama umeteketewa, umeliwa, umeangamizwa, lo lote lile, Mungu atakuleta pamoja na Kristo Yesu atakapokuja. Si lazima mkusanyike magharibi au ko kote. Po pote Bwana akuongozapo...

¹² Hata hivyo, ukijisikia unataka kwenda magharibi, hebu nifanye hilo dhahiri sana sasa, kabla sijaondoka. Sasa, ili...(Wananasa ujumbe huu? Wanaunasa? Vema.) Usiache nikwambie uende wapi. Kama ukijisikia kama unataka kuja magharibi, kuja magharibi. Kama unajisikia unataka kwenda mashariki, kaskazini, magharibi, kusini, nenda ambako Bwana anakokuongoza. Kila mtu anayefahamu hilo asema; "Amina!" [Kusanyiko linaitikia, "Amina! —Mh.]

¹³ Mimi siko kujaribu kumwambia mtu ye yote asiende wapi. Ukija Tucson, Arizona, ambapo naishi kwa muda mfupi wakati huu...Kama nilivyowaambia asubuhi hii, nina tamaa ya kwenda nyumbani bila nyumbani ya kwenda. Laiti ningalikuwa na mtu fulani, mahali fulani ambapo ningepaita nyumbani na niende. Ya...Usiku huu, kama ningekuwa na dolla elfu kumi na ningenunua mahali kwa ajili ya—na kuzitoa bure kwa ajili ya mahali fulani ambapo ningesema, "Hapa ndipo mahali ningetaka kupaita nyumbani," ningezitoa kwa moyo mweupe. Sina mahali po pote.

Ndugu Freeman, nadhani unanijua tangu nilipokuwa kijana; mi—mi—mimi ni mzururaji. Usiwe mzururaji; pata mahali fulani unapopenda na ukae huko; mngoje Bwana Yesu.

¹⁴ Lakini ukitaka kuja magharibi kule Tucson, Arizona, ninakoishi, umekaribishwa; nitafurahia kuwa pamoja nawe. Wewe u ndugu yangu, dada. Ningefanya lo lote duniani kukusaidia. Na—na ninyi nyote ambao mmekuja nje kule, nimejaribu vema nilivyoweza kuwafurahisha, na kuwaonyesha kila kitu nilichokijua, na kuwapeleka hapa na pale, kufanya kila niwezalo. Nanyi kila mara mmekaribishwa.

¹⁵ Lakini kama unakuja chini ya hali hizi, ukidhani kuwa Bibi-arusi au cho chote kile atanyakuliwa toka Tucson, Arizona, na pale pekee, umekosea. Usije kule kwa kusudi hilo, usije kwa kusudi hilo, kwa sababu hilo ni kosa. Hilo si sahihi.

¹⁶ Sasa, Ufunuo sura ya 12. . . Lakini jambo moja pekee Bwana analonifunulia au kuniambia mimi. . . Nimetoka tu kwa maono hayo (mwaona?) na ni vigumu kuyaondokea. Ona? Lakini yaonekana Yeye ananiambia tena nizungumzie zaidi juu ya huku kuenda magharibi.

¹⁷ Sasa, kama nilivyosema hapo mbeleni, mimi siko kule nje ili kuwa tu kule nje, niko kule nje kwa sababu naongozwa kuwa kule nje. Lakini kukaa kule nje, kupafanya nyumbani, nadhani hilo ni kosa. La, nadhani haitakuwa ila muda mfupi tu hadi kusudi ambalo Mungu amenituma kule litekelezwe. Siwezi kuwaambia ninyi hapa sababu ya kwenda kule, lakini singelienda kule bure.

¹⁸ Swali liliulizwa hivi majuzi: “Tunajua sababu gani ulienda kwanza kule Arizona, ilikuwa wakati Malaika wale walipotokea. Mbona ulirudi kule mara ya pili?” Mnakumbuka swali hilo liliposomwa?

¹⁹ Wangapi wanakumbuka niliporudi tena baada ya hayo nami nilikuwa nimeketi pale mbele ya Dk. Lee Vayle (naamini yeye yuko jengoni mahali fulani) na mke wangu? Nami nilikuwa nikiongea kuhusu Arizona na kuhusu sisi kuishi hapa, na pale kukaja mkono ukutani na nuru na kuandika maandishi haya. “Rudi tena Arizona.” Wangapi wanakumbuka hayo? Hiyo ndiyo sababu nimerudi kule tena. Bila kujua sababu gani nilirudi na nilipofika kule, ndipo Yeye alifunua sababu gani nikarudi kule. Nami nikinena hayo, Shetani atayazuia. Lakini yeye hajui moyo wangu. Yeye si Neno, kwa hivyo hajui moyo wangu. Lakini nikiyenena, ndipo yeye atayasikia. Kwa hivyo, kumbukeni hilo.

²⁰ Sasa, niliposema hivi majuzi, karibu nilifanye. . . Huenda mkapata wazo baya; nilisema, “Msije Arizona.” Sikukusudia, “Msije!” Lile lililokusudia lilikuwa: Ukiongozwa kuja, fanya hivyo basi, kama unaongozwa kuenda California, Arizona, ko kote uliko. Lakini kama ukienda kule, useme, “Ndugu Branham, ninaenda kule, kwa sababu naamini utakaa kule na kuhubiri Neno,” naamini umekosea pale. Ona? Mahali mahubiri yangu yaliko, ni papa hapa katika maskani haya; hapa ndipo.

²¹ Sina hata ibada moja kule Arizona. Nami siko Arizona ila kwa masaa machache tu kwa wakati mmoja. Sina. . . Nina mkutano wa Wafanyi Biashara baada ya Krismasi, mwanzoni mwa mwaka, kule Phoenix. Huo tu ndio nilio nao; niliahidi huo, hakuna mwingine.

²² Mkutano wangu unaofuata, kadiri nijuavyo, ni papa hapa kwenye Barabara ya Nane na ya Penn kwenye Maskani ya Branham. Nina masomo thelathini au arobaini ninayojua

yangechukua juma moja au mawili kwa wakati mmoja kuyamaliza, ambayo ninayo moyoni mwangu kuyahubiri hapa kwenye Maskani ya Branham, papa hapa Jeffersonville, Indiana.

²³ Na sasa, kama mnataka kabisa kuenda mahali fulani kukaa na Neno, ambapo Ujumbe wetu. . . Na Ujumbe wetu si tofauti, ni Ujumbe ule ule ambao umeusikia maishani mwako mwote, ila tu kitu fulani kimefunuliwa Kwake. Ujumbe huu ndio ule Luther alihubiri, Ujumbe ule ule ambao Wesley alihubiri, Ujumbe ule ule ambao Wapentekoste walihubiri, ila tu kitu fulani kimeongezwa Kwake. Hicho ni, ni kufunuliwa kwa zile Muhuri, ambazo hao watengenezaji waliacha (ona?), ambazo zimeelezwa katika siku hizi ambazo hazingalijulikana wakati huo. Ujumbe wa Kipentekoste haungelijulikana katika siku za Luther au Wesley; ilipasa ungoje hadi wakati wa Kipentekoste. Lakini wakati wa Pentekoste si kitu ila hatua nyingine ya wakati wa Kilutheri. Kama tu mahindi yanapoiva ama cho chote kile, vivyo hivyo na kanisa pia.

²⁴ Kama ningehubiri usiku huu, ningehubiri juu ya somo—nimetia alama hapa katika Biblia—*Ule Mzabibu uliokuwa umehamishwa kutoka Misri hadi Palestina*. Wangapi wenu mliwahi kujua kuwa Mungu alikuwa amesema Israeli walikuwa mzabibu Wake? Ndipo kutoka kwa hayo namtaja Yesu kuwa Mzabibu ule. Na Kanisa sasa limehamishwa ulimwenguni, haliketi katika uchafu, lakini linaketi katika Kristo, ambalo lapaswa kuzaa matunda. Mwaona? Na huo ulipaswa kuwa ujumbe wangu kwa ajili ya usiku huu kama ningalihubiri. Lakini nilidhani heri niyajibu maswali haya, kwa hivyo niliacha tu huo. Nitachukua huo labda nitakaporudi.

²⁵ Ufunuo sura ya 12 haimhusu Bibi-arusi. Ufunuo sura ya 12 (sijaichunguza bali najua), ni yule mwanamke anayeketi katika jua na mwezi chini ya miguuni yake. Mwezi uliainisha torati; mwanamke aliainisha Israeli, kanisa lile; na zile nyota kwenye paja la uso wake zilikuwa wale mitume kumi na wawili, nyakati kumi na mbili za kanisa, na kadhalika, ambazo tayari zimepita. Ona? Na jua lilikuwa kichwani mwake. Ambapo mwaona, mwezi ni kivuli cha jua, halafu torati ilikuwa kivuli cha mambo mazuri yajayo. Na mwanamke huyo ni Israeli, si Bibi-arusi.

Sasa sitachukua wakati mwingi sana, kwa sababu yanipasa niyamalize.

378. Warumi 7:14-18, “Kwa maana twajua torati asili yake ni ya rohani; bali mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi. Maana si—sijui nifanyalo, kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalotenda. Lakini kama nikilitenda lile nisilolipenda, naikiri (n-a-w-e-z-a) i—ile sheria, naikiri ile sheria, ya kuwa ni njema. Basi sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda

hilo, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu.” Haya siwezi kuyaelewa.

²⁶ Vema, waliandika Maandiko; hayo ni Paulo akiwazungumzia Warumi. Sasa yeye alisema...Hebu niyafafanue ili mpate kuyaona. Yeye alisema, “Ndani yangu mna watu wawili: mema, mmoja ataka nifanye; mabaya, yule mwingine anataka nifanye. Na kila wakati ninapoanza kufanya yaliyo mema, ndipo mabaya yanizuia.”

²⁷ Wangapi wenu watu kwenye mahojiano adhuhuri ya leo wamekabiliana na jambo lile lile asubuhi hii (ona?), jambo lile lile? Nilinena juu ya haya asubuhi hii, yasiyodumu.

²⁸ Wewe ni mtu wa nje unayesimamiwa na hisi sita; wewe u mtu wa ndani anayeongozwa na hisi moja ambayo ni imani. Na imani hii haikubaliani na zile hisi zote sita kama zile hisi sita hazikubaliani na imani. Lakini moja ni kinyume cha nyingine. Sasa mradi tu hizo hisi sita zinakubaliana na imani, sawa kabisa; lakini hizo hisi sita zisipokubaliana na imani, ndipo achana na hizo hisi sita.

²⁹ Sasa, kwa mfano hapa, Yesu alitoa matamshi, ahadi. Mtu wa ndani asema hayo ni kweli; mtu wa nje anapobishana kuwa haiwezi kuwa kweli kwako, basi usimjali yule mtu wa nje kisha mkubali yule mtu wa ndani. Sasa, hili ni jambo lile lile analonena Paulo. Yeye aliuzwa chini ya sheria kwa dhambi ya kimwili. Kila mmoja wetu yu vivyo hivyo. Hiyo ndiyo sababu sisi tuna—tuna shida tulizo nazo, za kuoana mara nne au tano, na *hii*, na *ile*, na *ki*—kila dhambi ya kila namna, na uzinzi, na kila kitu kote maishani mwetu, ni kwa sababu ya mambo hayo. Sisi tu wa kimwili, na sehemu hiyo haina budi kuangamia; lakini basi, mle ndani, sisi ni watu wa rohoni, nafsi iliyo mle ndani, na hiyo ni imani katika Neno la Mungu; ndipo tunaleta mwili wetu wa nje chini ya utiifu wa Neno kwa imani, kwa kukubali yale Mungu aliyosema.

³⁰ Naweza je kuchukua gugu na nifanye punje ya ngano kwake? Siwezi kufanya hilo. Njia pekee inavyowezekana ni kwa sababu ndani ya gugu hilo kumegeuzwa toka kwa gugu kuwa ngano—gugu kuwa mche unaoitwa “uhai wa ngano.” Ndipo unazika gugu hilo, na litazaa punje ya ngano (naam, ona?), kwa sababu kuna uhai wa ngano uliowekwa ndani ya hilo gugu. Na ule uhai wa gugu umeondolewa; bali ile tabia ya gugu ingali inanata (ona?), na itakuwa hivyo hadi maisha haya mapya yameumbika kabisa toka ardhini na kuota tena. Yanapochipuka, ndipo si gugu tena, lakini ni ngano—lakini ngano. Lakini iwapo hapo duniani na ile—katika—toka ardhini... Nalo gugu, lingali linanata, lakini ndani yake lina asili ya ngano.

³¹ Na mradi tu wewe umo katika maisha haya, utakuwa wa kunata na kuwa na tabia ya mwilini itakayokutatiza mradi tu u hai; lakini ndani yako, umezaliwa mara ya pili. Na

utakapofufuliwa, wewe uko katika mfano wa Kristo na dhambi zote zimekuondokea. Ona? Hivyo—hivyo ndivyo ilivyo.

³² Na niseme hili? Inaokana kama mzaha. Mhindi Mwamerika fulani. Ni watu wa kuchekesha mno. Nami... Wao si wa kuchekesha; ni wa kushangaza kwetu sisi; lakini wanaonekana sawa wao kwa wao. Na ukiwajua, wao ni sawa. Mhindi aliulizwa siku moja alipookoka...

³³ Nakumbuka mmoja kule Phoenix, Arizona, Billy alikuwa akienda kusambasa kadi za maombi. Yeye kila mara husimama pale na kusambaza kadi za maombi. Na watu wale wanaoweza kukimbia juu pale na kunyakua zile kadi za maombi... Hali wale—wale watu waliokuwa wazima kweli walioumwa na kichwa, kuumwa na meno au wanaumwa na vidole vyao, walipata—walipata kadi za maombi, Ndugu Ruddell. Nao walipo—walipozipata, basi katika mstari wa maombi, jambo pekee nililopata, mtu fulani anaumwa na kichwa, mtu fulani hawezi kidole cha mguu, na mambo kama hayo. Na kulikuwa na watu walioketi pale wakifa kwa ugonjwa wa kansa na kadhalika ambao hawakujaliwa kuingia katika mstari wa maombi. Nilisema, "Billy, nenda chini kule ukawaulize wale watu shida yao. Na iwapo hawana kansa, au ugonjwa fulani mbaya, au kitu fulani kitakachowaua, usiwape kadi za maombi. Walete watu juu pale katika mstari wa maombi ambao wata—ambao wako karibu kufa wasiposaidiwa na Bwana. Acha wengine wangoje. Acha waje kwa mstari uanoenda upesi au cho chote kile. Lakini waruhusu watu wanaokaribia kufa..." Nilisema, "Waulize."

Yeye alisema, "Vema, ulisema, 'Changanyisha tu kadi hizo na kuzisambasa,' hayo ndiyo niliyokuwa nikifanya."

Nilisema, "Lakini unawafanya hao watu—unakimbia juu pale mbele yao, nao wanapata... Hao maskini viwete na kadhalika hawawezi kuzipata."

"Vema, nitafanya hivyo."

Yeye akashuka akaenda kule; kulikuwa na Mhindi mzee—nao ni wa kushangaza sana—yeye hangeketi kitini. Walimpa kiti, lakini aliketi sakafuni hemani. Yeye alikuwa amevaa kofia; naye hangeitoa; ilikuwa na unyoya uliopepea nyuma yake, ameketi tu pale.

Billy alimwendea naye akapitia karibu naye, naye akasema, "Unahitaji kadi ya maombi?"

"Hmm."

Yeye alisema, "Una shida gani, Chifu."

Yeye akasema, "Mimi gonjwa?"

Akasema, "Lakini shida yako ni nini?"

Akajibu, "Mimi gonjwa!"

Akasema, “Lakini nataka kujua una shida gani?”

Akasema, “Mimi gonjwa!”

³⁴ Ni hayo tu ndiyo angepata toka kwake, kasema, “Vema, nitarudi baada ya kitambo kidogo.” Kwa hivyo Billy akaendelea kuuliza watu. Yule Mhindi alizidi kutazama hizo kadi za maombi zikiendelea kupunguka. Kila wakati yeye angezitoa mfukoni mwake zilikuwa chache zaidi. Kwa hivyo baada ya kitambo kidogo, yule Mhindi mzee aliamka, akaenda pale, na kumgusa Billy nyuma kumkumbusha yeye alikuwako pia. Yeye alisema—yeye alisema, “Chifu una nini?”

Yeye kasema, “Mimi gonjwa!”

Akasema, “Vema, Chifu, yakupasa uniambie. Baba aliniambia nisiwape kadi hizi watu ambao wange—walikuwa tu, kama kusokotwa na tumbo, na kuumwa na kichwa, na kadhalika. Wape watu ambao ni wagonjwa mno.” Kasema, “Unaumwa wapi chifu?”

Yeye alisema, “Mimi gonjwa.” Yeye alimketisha chini tena kabla yeye—kadi zake zilikuwa karibu kwisha. Dakika chache (yeye alizidi kuziangalia zile kadi.) Yeye alirudi na kumgusa tena. Yeye...?...basi. Billy aliweka kadi ile mkononi mwake, kasema, “Chifu, nenda andika mle juu, ‘Mimi gonjwa.’”

³⁵ Yeye aliingia katika mstari wa maombi, nami nilikuwa nikimwombea, nami nilimwuliza, “Je, unaamini, Chifu?”

Yeye kasema, “Hiyo kweli.”

Nami nikamwambia, “Vema, unaamini kuwa Mungu atakuponya?”

Yeye kasema, “Hiyo kweli.”

Nilisema, “Utakuwa mvulana mzuri?”

Yeye kasema, “Hiyo kweli.”

Nilikutana naye yapata juma moja baadaye. Ndugu Fred Sothmann naamini alikuwa pale. Ilikuwa wakati wao—na wakati mkutano wa hema ulipokuwa ukiendelea. Ilikuwa kule Phoenix. Nami nilikutana naye baadaye juma lile; nikasema, “U hali gani, Chifu?”

Yeye akajibu, “Hiyo kweli.” Nikatambua, niliongea na... Jina la mumishenari huyo lilikuwa nani juu pale, yule mzee mwenye masharubu meupe, juu pale kwa Apache? Sikumbuki jina lake. Vema, yeye ni mtu mzuri. Mkewe aliponywa ugonjwa wa kansa, mwajua. Yeye alisema, “Ndugu Branham, hayo tu ndiyo anayoweza kusema.” Kasema, “Nilimfundisha kusema, ‘Mimi gonjwa.’ Hilo tu ndilo neno analoweza kutamka, ‘Hiyo kweli.’” Kwa hiyo ni—ni hayo tu, mwaona. “Hiyo kweli. Mimi gonjwa!”

³⁶ Mtu fulani aliniambia alikuwa na mmoja, wakati mmoja akaongoka, akampokea Roho Mtakatifu, naye akamwambia, “Unaendeleaje?”

Naye alisema, “Vema sana na vibaya sana.”

Yeye alisema, “Vema, unamaanisha nini kwa vibaya sana na vema sana?”

Yeye akasema, “Vema, tangu kupokea mimi Roho Mtakatifu,” yeye alisema, “kumekuwa na mbwa wawili ndani yangu, na mmoja wao ni mbwa mweusi na mwingine ni mbwa mweupe.” Akasema, “Wanabishana wakati wote.” Kasema, “Wanangurumiana na kupigana.” Kisha akasema, “Yule mbwa mweupe ananitaka mimi nifanye mema; na yule mbwa mweusi ananitaka nifanye mabaya.”

Kasema, “Vema, Chifu, ni nani anayeshinda vita?”

³⁷ Kasema, “Hiyo inategemea yupi Chifu anayemlisha sana.” Kwa hivyo nadhani hilo ni jibu nzuri hapa. Ona? Inategemea tu vita vya mwilini mwako; inategemea ni yupi unayemshughulikia, ni tabia gani unayoishughulikia, ile tabia ya kimwili inayopenda mambo ya ulimwengu, au ile tabia ya kiroho inayopenda mambo ya Mungu. Ndivyo ilivyo.

379. Je, kila mwana wa Mungu aweza kutiwa mafuta sana hata yeye aweze kufanya miujiza, ishara, maajabu, au hili ni—je, hili ni kwa uongozi wa Roho Mtakatifu?

³⁸ Naam, ni kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu. Kama wewe ni mwana wa Mungu, au binti wa Mungu, vyo vyote ulivyo, unapompokea Roho Mtakatifu, basi Roho Mtakatifu anakuongoza kutenda mambo.

³⁹ Sina wakati. Laiti ningeliwasimulia hadithi ndogo. Kila wakati ninapowaza habari zake, yanipasa tu kuiacha. Lakini nafikiri hii itachukua dakika moja hivi.

⁴⁰ Ilikuwa kule Meridian, Mississippi, wengi wenu watu wa oneness, Ndugu Bigby alikuwa akishikilia—alikuwa akigharimia mikutano yangu, yeye ni ndugu wa oneness. Na usiku mmoja mkutanoni, Billy Paul alikuwa ameenda kote uwanjani na kusambasa kadi za maombi. Basi, kulikuwa kunanyesha. Na watu walikuwa wamesimama nje wakiwa na miavuli na kadhalika. Basi Billy akasambasa kadi za maombi, na alikuweko... Kisha akaja kunichukua. Na tulipokuwa huko alikuweko—alipokuwa akija kunichukua, alikuweko maskini bibi mmoja aliyeketi hapo mbele na kulikuwa na bibi mwingine akitembea na mtoto mchanga, akijaribu kumnyamazisha. Na maskini bibi huyo alikuwa ameketi pale hali amevalia nguo ya kaniki, cho chote kile, alikuwa mama pia. Naye alimwona bibi yule, kisha Roho Mtakatifu akanena na mwanamke yule, kitu fulani moyoni mwake, “Nenda kamwombe yule mtoto mchanga.”

⁴¹ “Vema,” yeye alisema, “atakapopita tena, nitaenda kumwombea.” Na yeye alipopita tena, mwanamke yule alikuwa anashikilia kadi ya maombi. “Ee,” yeye alisema, “Si—singemwombea huyo mtoto mchanga.” Kasema, “Ndugu Branham atamwombea mtoto huyu usiku huu. Na mimi ni nani hata nimwombee mtoto huyu kama Ndugu Branham atamwombea?” Sasa, hiyo ilikuwa heshima, na hilo lilikuwa nzuri, lakini hilo kila mara haliwezi kuwa mapenzi ya Mungu. Wakati mwingine ni tofauti.

Roho Mtakatifu alizidi kumwambia, “Nenda kamwombee mtoto huyo.”

Hatimaye yeye alidhani, “Mwanamke huyo hatanisikiza. Akijua yeye ana kadi hiyo ya maombi, yeye hataniruhusu mimi nimwombee mtoto huyo. Yeye alimleta mtoto huyo hapa, si ati nimwombee mimi, bali Ndugu Branham amwombee.”

Kwa hivyo Roho Mtakatifu alizidi kumwambia, “Nenda kamwombee huyo mtoto mchanga.”

Mwishowe yeye kasema, “Vema, kusudi nikajitulize nitasema tu. . . Nitampa kiti changu.” Kwa hivyo yeye alisema, “Mpenzi (maskini mama mmoja akiongea na mwingine), je u-ungetaka. . . Una mtoto huyo mchanga. . .” Kasema, “Je, waweza kuja, uketi hapa, uchukue kiti changu?”

Yeye kasema, “Ee, mpenzi, sitaki kuchukua kiti chako.” Kasema, “Ninajaribu kumnyamazisha mtoto.”

Kasema, “Lakini unaonekana mchofu mno na mlegevu.”

Yeye kasema, “Naam.”

Yeye kasema, “Vema, keti hapa uchukue kiti changu.” Naye akasema, “Nakuona una kadi ya maombi. Labda una—Ndugu Branham atamwombea mtoto wako?”

Akasema, “Tunatumai kuwa nambari hii itaitwa.”

Naye kasema, “Vema, nami pia.” Yeye kasema, “Dada, wewe u Mkristo?”

Kajibu, “Ee, naam!”

Yeye akasema, “Mimi pia ni Mkristo.” Kisha akasema, “Tangu nilipoketi hapa, Roho wa Bwana amekuwa akiniambia mimi, ‘Ombea mtoto huyu.’ Je, waweza kuniruhusu? Najua Ndugu Branham atamwombea mtoto huyo kama ikiitwa. Nawe endelea tu kushikilia kadi yako, yeye ataifikia.” Kasema, “Lakini nikiweka mikono yangu juu ya mtoto huyu, na kuomba tu maombi madogo kuridhisha nafsi yangu, nami nikiondokee hicho kinachoniita, je—je, lingekuudhi?”

⁴² Yeye kasema, “Naam, hakika sitaudhika, Mpenzi. Mwombee mtoto huyu.” Na alikuwa ni mtoto mwenye macho ya samawati, na kwa hivyo maskini yu—yule mama akamwombea. Akampa mwanamke yule kiti chake, naye akapanda katika roshani ya

tatu akasimama. Ndugu fulani Mkristo juu pale, mwungwana kutosha akasimama na akampa mwanamke huyu kiti, kwa hivyo yeye akaketi chini.

⁴³ Yapata nusu saa baadaye, niliingia mkutanoni, nikazungumza kwa dakika chache, nikaita kadi za maombi; na mwanamke huyu alikuwa wa tatu au wa nne mstarini akiwa na mtoto huyo. Naye aliketi pale, naye kasema, “Ee, asante, Bwana. Sasa, nilimsikitikia sana maskini mama huyo, naamini mtoto huyu atapona sasa, kwa sababu Ndugu Branham... Wa tatu au wa nne tu, yeye atamfikia huyo.” Kasema, “Asante, Bwana,” maskini mama yule akiketi pale, akimsikitikia yule mtoto. Vema.

⁴⁴ Ndipo nilipokuja, nikaanza kumwomba mtoto huyo, mama yule alipokuja, kasema, nilimtaazama nikasema, “Sasa, mtoto wako ana macho ya samawati; na ulimleta hapa aombewe. Na sasa, jina lako ni Bi. *Fulani*, na unatoka mahali paitwapo *hivi na vile*, lakini huyo mtoto amekwisha pona. Kulikuwa na mwanamke aliyekuwa na mzigo moyoni mwake jina lake Bi. *fulani*, anayeketi juu pale kwenye roshani (wa kwanza katika mwisho wa mstari wa nne katika roshani ya tatu), aliomba ombi la imani kwa ajili ya mtoto huyu; na mtoto huyo amekwisha pona.” Karibu aanguke toka kitini. Ona?

⁴⁵ Sasa, vipi kama yeye hangelikuwa amefanya hilo? Mnaona ninalomaanisha? Naam, wanawake hao wangemsikitikia mtoto huyo, mama kwa mtoto kuliko vile ningemsikitikia mtoto huyo. Ona? Na mama akiwa... Ona?

⁴⁶ “Je, sisi sote twaweza kufanya miujiza?” Naam. Unapoongozwa na Roho Mtakatifu kufanya miujiza, nenda kaifanye, kwa sababu umeongozwa na Roho Mtakatifu.

⁴⁷ Sasa, kama mwanamke huyo hangetekeleza yale Mungu alimwambia, labda kungekuwa na kukemewa katika Roho kwake (mwaona?), naye angekuwa amekataa kumtii Mungu. Kila mara, kama wewe u Mkristo na kitu fulani kinakushawishi wewe kufanya jambo fulani, nenda kafanye. Nenda kalifanye; usitie shaka; nenda kalifanye.

“Ningependa kuuliza swali. Je...” Hapa kuna lingine layo, au labda sikulipata vilivyo... Naam, mimi—hilo ni la asubuhi ya leo. “Wanawake kuvaa suruali ndefu za kutumia wanapolala, je, ni vazi la mwanamume?” Halina budi lilichanganyikana hapa katika haya mengine.

“Ndugu Branham, je, Mungu alikuwa akifanya jambo—je, Mungu—nilikuwa nikifanya jambo lile lililotendeka wakati ile kanda...” Ee, naam, tulikuwa nalo asubuhi hii. Sina budi nimeyachanganyisha haya. Yanipasa niyararue, lakini nachukia kufanya hivyo.

380. Ndugu Branham, kina nani watakaoijaza nchi nje ya ule Mji wa Kimbinguni?

381. Eleza juu ya malaika wa kila mtu ambaye hukaa pamoja nao tangu wanapozaliwa hadi wanapokufa. Swali nzuri sana.

⁴⁸ Nachukia kuyaacha haya; ni maswali mazuri. Nami nataka watoto wa—wangu wajue mambo haya. Ona? “Sasa, nani watakaojaza nchi nje ya Mji ule?”—nje. Waliokombolewa ndio watakaojaza nchi hiyo nje ya Mji ule, lakini hawatakuwa wale Bibi-arusi aliyeteuliwa na aliyetitwa. Bibi-arusi ataishi ndani ya ule Ufalme pamoja na Mfalme. Upande wa nje kutakuwa na wafalme wa nchi watakaofanya kazi na kuleta bidii zao—kuleta—si bidii, lakini kuleta matunda yao katika Mji ule. Na milango haitafungwa usiku.

⁴⁹ Sasa, juu. . . Sasa, Nuru hii juu ya mlima haitaangaza dunia nzima, itaangazia tu Mji ule. Lakini labda yaweza kuonekana umbali wa maili elfu kadhaa; lakini haitaangazia dunia, kwa sababu Biblia ilisema, katika ile Nchi Mpya, ya kuwa toka Sabato moja hata nyingine na toka—toka mwezi mpya hadi mwingine (mwaona?) watu watapanda waende mbele za Bwana kule Sayuni—kwenye Mji ule kuabudu.

⁵⁰ Na sasa, watakuwa nje ya Mji ule, si yule Bibi-arusi, lakini watu watakaokuja katika ule ufufuo wa pili watakaokuwa wakulima, kama tu Adamu alivyokuwa, na kadhalika, na watunza bustani. Lakini yule Mfalme pamoja na Malkia watabaki katika Mji ule.

⁵¹ “Eleza juu ya malaika wa kila mtu anayekaa pamoja nao tangu wanapozaliwa.” Sasa, ukichunguza. . . Sasa, hili ni la kilindi mno. Sasa, sikuwahi kamwe—nililichukua tu. Sasa, lile. . . Sehemu yake imepigwa chapa na ile nyingine imeandikwa kwa penseli—au kalamu ya wino.

⁵² Sasa, kuna Malaika, lakini Malaika hawa wa Bwana wanaofanya kituo kuwazunguka wale wawachao—wale wamchao. Ona? Sasa, haijaahidiwa kuwa wenye dhambi wana Malaika, ni wale tu waliokombolewa walio na Malaika. Je, mlijua hilo? Malaika wa Bwana hufanya kituo wakizunguka wale wanaomcha Yeye.

⁵³ Sasa, Malaika ni wajumbe. Sasa, nataka ninyi mtambue. Ni kamili sana, na litawathibitishia kule kuchaguliwa tangu awali. Ona?

⁵⁴ Sasa, mtoto mchanga anapoubika chini ya moyo wa mama yake. . . Nanyi watoto wadogo mnaofahamu mambo haya, ona, Bwana aliwatolea ninyi kwa mama. Naye akawabeba chini ya moyo wake, kwa sababu wewe u karibu na moyo wake. Ndiposa, siku moja Bwana akashuka na kuwatoa ninyi toka kwa moyo wa mama, toka mle ndani kabisa ya moyo wake, lakini wewe kila mara utakuwa moyoni mwake.

⁵⁵ Sasa, wakati mwili huu mdogo unapoubika, mwili huu mdogo wa kawaida unapoubika ndani ya mama, kunao mwili

wa kiroho wa dunia hii tayari kuupokea huu mwili wa kawaida mara tu uzaliwapo. Sasa, mtoto mchanga huzaliwa na misuli hai, moyo unaodundadunda, lakini hamna pumzi ya uzima ndani yake. Ni misuli inayotetemeka. . . Ona? Ndipo, ona, kama kungekuwa na kitu fulani tofauti na hicho, kama hakungekuwa na roho ambayo ingeingia ndani yake baadaye, basi pumzi yetu ingetuondoka, nasi hatungepumua tena na bado tuwe hai. Lakini mwili huu kama haupati hewa ya oksijeni toka kwa—au pumzi (kupumua na kupuliza kwa mapafu), basi tumekufa.

⁵⁶ Sasa, lakini wakati mama. . . Mtoto mchanga anaposhuka duniani toka kwa moyo wa mama (“kushuka,” mwafahamu ninalosema, jinsi mimi—sababu ya kusema hivi), mtoto mchanga anaposhuka, nini hutendeka? Mara tu anapozaliwa, kama haanzi kulia, daktari, mzalishi, au ye yote yule, atampiga [Ndugu Branham apiga makofi—Mh.] kumnyosha. Hana budi kugutuka, basi nini hutendeka?

⁵⁷ Tazama, mama, yeye aweza kuwa mchoyo sana na mkali, lakini kabla tu mtoto huyo mchanga hajazaliwa, kuna namna fulani ya wema inayoingia. Je, uliwahi kumtazama mama anapokaribia kuwa mama? Kuna kitu fulani kizuri kumhusu; yeye kila mara huwa na uzuri huo. Ni kwa sababu huyo—huyo malaika mdogo, roho mdogo, mjumbe mdogo kwa haya maskani madogo yu tayari kuzaliwa duniani. Ndiposa, huyu malaika mdogo anapoingia katika huo mwili (huyo ni malaika mdogo wa duniani, roho aliyechaguliwa na Mungu kuchukua mwili huu), ndipo huyo mtoto mchanga hana budi kujichagulia. Hukata kauli. Ndipo hili litendekapo, basi unamwona Malaika wa Bwana sasa akiingia humu ambaye ni mwili wa kiroho, ule wa milele.

⁵⁸ Hii ni roho inayokufa katika mwili unaokufa; lakini sasa, huwezi kuwa katika miili miwili kwa wakati mmoja, lakini kunaweza kuwa na tabia mbili ndani yako kwa wakati mmoja. Sasa, ile tabia ya Roho wa Bwana. . . Unapozaliwa mara ya pili, huzaliwi kwa mwili, kama azaliwapo mtoto mchanga; lakini kile kinachotendeka, unapata kuzaliwa kwa roho. Na wakati huku kuzaliwa kwa roho kunakua katika moyo wako, wa Mungu, kuna mwili wa kawaida au wa kimbinguni unaokua upate kuipokea roho hiyo. Na uhai unapouacha mwili huu, unaenda kwa mwili huo. Kama tu vile mwili unapotolewa duniani, roho anaingia, basi roho aondokapo mwilini, kuna mwili unaongoja. “Kwa kuwa twajua nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibika, tunalo jengo lingine linalotungoja.” Ona? Naam, ule mwili wa kiroho wa watu.

Ndugu Branham. . .

Sasa, haya hayana budi kuwa. . . Kuna kundi layo hapa, yaonekana kama yasiyopungua kumi au kumi na matano. Yote yameandika kwenye karatasi, karatasi ya aina moja, yamepigwa

chapa, na kadhalika. Nitajaribu kuyafikia upesi niwezavyo. Tunaweza kuondoka katika—upesi iwezekanavyo.

382. Mpendwa Ndugu, Yesu hangekubali kusujudiwa na Yohana katika Ufunuo yeye alipoanguka...Mbona Yesu hangekubali kusujudiwa na Yohana katika Ufunuo Yeye alipo—hali Yeye aliruhusu kusujudiwa mbele yake? Mbona Yesu hangekubali kusujudiwa wakati Yohana alipotaka kumsujudia?

⁵⁹ Ndugu au Dada yangu mpendwa, ye yote yule, haikuwa Yesu ambaye alikataa kusujudiwa. Katika Ufunuo 22:8, utasoma ilikuwa nabii, malaika, ambaye hangekubali kuabudiwa. Yohana alipoanguka chini kumsujudu malaika ambaye alikuwa amemwonyesha mambo haya, yeye alisema, “Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako. Mimi ni mmoja wa manabii.” Ona, ona? “Mimi ni mjoli wako, mtumishi mwenzako, mmoja wa manabii; msujudie Mungu.” Si Yesu ambaye hakukubali kusujudiwa, ni nabii ambaye hangekubali hayo.

383. Mpendwa Ndugu Branham, nini tofauti Yesu alipowapulizia wanafunzi, akasema, “Pokeeni Roho Mtakatifu,” na hata hivyo wao—ilipowabidi waende kwa chumba cha orofa kungoja?

⁶⁰ Ilikuwa ni ahadi aliyowapa, akawapulizia ahadi Yake, kasema, “Pokeeni Roho Mtakatifu.” Ilikuwa ahadi. Wao walienda kwa kile chumba cha orofa kungoja, ile ahadi itimizwe.

⁶¹ Ni jambo lile lile tunapowawekea mikono kuponywa kisha mnaendelea na shughuli zenu mkingoja ahadi ile itimizwe.

384. Ndugu Branham, Je, Yesu alibadili vinyago vya mwili Wake mara kadha alipokuwa akiwatokea wanafunzi Wake baada ya kufufuka Kwake?

⁶² “Je, Yeye alibadili kinyago cha mwili Wake?” Si—singejua, kwa sababu nadhani ilivyokuwa; Yeye hakubadili kinyago Chake pale. Jambo alilofanya, Yeye alikataa wasimwone au wasimtambue.

⁶³ Kama wale waliotoka Emau, walitembea pamoja Naye siku nzima nao wakafumbwa macho. Nao walimwona mtu ukingoni wakati mmoja akivua samaki ambapo walikuwa tayari wamevua; Yeye akasema, “Watoto, mmepata cho chote?”

Nao wakajibu, “Hatujavua kitu, tumefanya kazi usiku kucha.”

Yeye akasema, “Litupeni upande mwingine.” Nao wakashika samaki wengi mno, nao wakajua basi ilikuwa ni Bwana. Nadhani si kinyago Chake kilichobadilishwa, nafikiri ilikuwa tu ni macho ya watu yaliyofumbwa yasimtambue.

385. Ndugu Branham, nini tofauti, kama —kama kunayo ye yote, kati ya Malaika wa Bwana na Bwana, Mwenyewe.

⁶⁴ Malaika wa Bwana ni mjumbe toka kwa Bwana, na Bwana Mwenyewe ni Mtu huyo, si ule utu wa malaika, malaika toka kwa Bwana. Hebu niwaonyesheni. Kunena kidunia huyu ni malaika toka kwa Bwana. Kunena kidunia huyu hapa ni malaika toka kwa Bwana, tunajua basi kuwa ni malaika toka kwa Bwana? Wanapoleta Neno la Bwana. Lakini wanapojaribu kulipotosha, hawatoki kwa Bwana basi (ona, ona?)—kujaribu kulifanya kitu fulani lisichosema. Kusema tu vyo vyote. . .

⁶⁵ Ndipo kuna Malaika wa kimbinguni anayeshuka toka kwa Bwana, Mjumbe kama Gabrieli, na—na Mikaeli, Pakanga, na wengineo, majina yao.

386. Ndugu Branham, imekuwaje siku hizi tunazoishi, unapokuwa mwamini anayefuata Ujumbe na mjumbe wa siku hizi, huku haonekani kama unaweza kuomba kama vile ungependa kuomba? Hilo ni swali nzuri.

⁶⁶ Naamini Ndugu, Dada, ye yote uliyeuliza, ni kwa sababu ya hali za wakati huu. Ufufuo tayari umekwisha. Ufufuo umedumu kwa miaka kama kumi na mitano, na haukuwa kamwe hapo mbeleni umedumu kwa zaidi ya miaka inayozidi mitatu. Naamini imepokea ufufuo wake wa mwisho. Pia naamini hiyo ndiyo sababu hamwezi kuomba na kujisikia katika Roho kama mlivyokua mkijisikia. Ni kwa sababu mioto ya ufufuo imezimika.

387. Ndugu Branham, tafadhali eleza jinsi mtu anavyojua kama yeye anawaza nia zake mwenyewe, au kama shetani anaweka mawazo katika nia yake kumfanya yeye awazie vibaya, hasa, kama unajua hutaki kuyawaza.

⁶⁷ Basi, kama ni kinyume cha Neno, ni wazo la shetani. Kama ni sawa na Neno, ni Mungu anayewaza. Kama ni mawazo mabaya, ni shetani. Kama ni mawazo mazuri ya Neno na la Mungu, ni mawazo ya Mungu.

388. Iwapo shetani anaweka mawazo niani mwako kuhusu mambo fulani, unawezaje kuyashinda au kuyaondoa?

⁶⁸ Chukua kinyume cha hayo. Kama shetani anakufanya wewe uwaze kuwa—kuwa—kuwa wewe una. . . Kama unajua wewe ni Mkristo, naye anajaribu kukufanya ufikiri kuwa wewe si Mkristo, chukua tu kinyume chake, useme, “Mimi ni Mkristo.” Mradi matendo yako yanalingana na yale Neno la Mungu lisemayo, useme, “Mimi ni Mkristo.” Cho chote kile, vivyo hivyo.

Unapojibu hili, tafadhali niombee kushinda hili, kwa sababu mimi sijiwezi.

⁶⁹ Mungu na akupe ushindi wako, ye yote uliye. Na nia zako zirudi upande mwingine na useme, “Mimi ni Mkristo; Mimi ni mwamini. Shetani huwezi kunishikilia.”

⁷⁰ Hakika, ninasimama papa hapa sasa nikisema jambo lile lile, nisije nikazimia papa hapa mimbarani. Hiyo ni kweli. Mara nne au tano nusura nianguke hapa mimbarani. Hilo ni kweli. Mungu ajua hilo ni kweli.

389. Mtu anapotambua ana kinyongo cha kujidhili, au tabia fulani, yeye awezaje kushinda hili? Kwa hivyo—je, inawezekana kwamba kilichosababisha hayo ni kwamba yeye alikuwa mtoto wa pekee katika ujana wake?

⁷¹ Chukua msimamo kinyume cha hayo hasa. Kama wewe kila mara hutaka kupata haja yako, nawe ni mtoto mtukutu anayetaka kila mara kupata haja yake daima, geuka upande mwingine na utoe kila kitu ulicho nacho upande huo mwingine. Kama una uchoyo na unataka kushikilia kila kitu, basi anza kutoa ulivyo navyo. Ona? Fanya cho chote—enda tu kinyume. Hivyo ndivyo unavyoshinda cho chote ni dawa yake.

⁷² Una... Mama yangu mzee wa kusini alizoea kusema, “Manyoya ya mgongo wa mbwa ni mazuri kwa kuliwa.” Na hilo linafaa kwa haya pia.

390. Ndugu Branham, ni mafanikio gani ambayo tungewaachilia watoto wetu ambao hawajabalehe kushiriki: (Samahani, ni)—Ni shughuli gani watoto wetu wasiobalehe wanapaswa kutazamia—kushiriki katika shughuli gani. Pia yatupasa tuwasaidieje kuchagua wenzi wao?

⁷³ Wadumishe kwenye marafiki Wakristo kadiri uwezavyo. Wadumishe pamoja na... Iwapo ni msichana, mweke pamoja na wasichana Wakristo; wavulana Wakristo, vivyo hivyo. Kama msichana amefikia umri wa kutosha kuambatana na mvulana, ona kwamba anaambatana na mvulana mwema. Mshauri asiambatane na mvulana asiyefaa, au mvulana kwa msichana. Kama msichana yule anafanya uchumba na asiyeamini, jaribu kumshauri apozwe na mwamini, na kadhalika. Fanya nyumbani kwako kuzuri. Fanya nyumbani kwako mahali ambapo binti yako na mwanao hawataaibika kuleta wenzi wao mbele ya baba na mama yao, na nyumbani mwao; na fanya nyumbani kuzuri sana hata watafurahia kukaa nyumbani mwao.

Salale, mama wee, hapa kuna saba mfululizo. Sitaendelea ila kwa dakika chache zaidi.

391. Ndugu Branham, je, umetoa matamshi hivi majuzi kuwa wakati wa kanisa umekwisha, Laodikia?

⁷⁴ La, sikusema kamwe umekwisha. Kama nilifanya hivyo, ulinifahamu kwa kosa, ama nilisema vibaya. Ni—huu ni wakati wa mwisho wa kanisa; ni mwisho wa nyakati za kanisa, huu wa Laodikia. Haujakwisha; utakapokwisha, Kanisa limenyakuliwa. Kwa hivyo mradi Kanisa liko hapa, haujakwisha. Ona?

392. Je, wakati wa kanisa umekwisha na ukatiwa giza, Bibi-arusi ameitwa, tumekwisha ingia katika ule wakati wa ile dhiki?

⁷⁵ La, hashia, hapana, wewe . . . Laiti ningalikuwa tu na wakati zaidi kwa hilo. Ona, ona? Bibi-arusi, Yeye atakapotwaliwa toka kanisani, basi wakati wa kanisa utakoma. Laodikia itaingia katika mchafuko; Bibi-arusi ataingia Utukufuni; na ule wakati wa ile dhiki utanza juu ya wale wanawali waliolala kwa miaka tatu na nusu huku Israeli inapata unabii wake; kisha ile dhiki itakuja juu ya Israeli; halafu vitaanza vile vita vya Amagedoni vitakavyoharibu vitu vyote. Ndiposa, Bibi-arusi atarudi tena pamoja na Bwana arusi kwa miaka elfu, ule Utawala wa Miaka Elfu; baada ya hayo inakuja ile hukumu ya kile Kiti cheupe cha Enzi; baada ya hayo itakuja Mbingu Mpya na Dunia Mpya na ule Mji Mpya ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu. Milele na wakati vinachanganyikana.

393. Roho Mtakatifu amekwambia kuwa zile Baragumu hazihusiani na Bibi-arusi. Je, vile Vitasa Saba vina uhusiano wa wote nasi?

⁷⁶ Nitangoja nione kama Roho Mtakatifu atanifunulia kwa njia hiyo. Sijui bado.

394. Je, yule nabii wa Malaki 4 ndiye atakayeita yale mabaki ya Mataifa ya Ufunuo 7:9, ijapokuwa wanapitia katika ule wakati wa ile dhiki?

⁷⁷ La, hapana! Baada ya—ya Ufunuo 7, ndipo yeye aliona wale 144,000 waliotiwa muhuri, na baada ya hayo yeye aliona lile kundi kuu likijitokeza, kundi kubwa likirudi ambalo hakuna mtu angelihasabu ambalo lilikuwa yule Bibi-arusi. Litakuwa . . . Lile . . . Malaki 4 itatimia kisha Bibi-arusi atanyakuliwa, halafu lile—ndipo lile—hili kundi la—la Eliya na Elisha litarudi tena duniani kwa ajili ya . . . Kanisa kupitia katika ule wakati wa ile dhiki iliyo kuu, lakini Eliya na Elisha hawatahusiana kwa lo lote lile na wale wanawali waliolala (wao ni Mataifa); watapelekwa kwa Wayahudi pekee.

395. Je, zile Ngurumo Saba ambazo ni sawa na siri saba zimekwisha kufunuliwa? Je, zilifunuliwa katika zile Muhuri Saba, ila bado—ila bado hazijajulikana kwetu kama Ngurumo?

⁷⁸ La, zilifunuliwa katika zile Muhuri Saba; hivyo ndivyo zile ngurumo zilivyokuwa. Ilibidi zifunue . . . Zile Ngurumo Saba zilizotoa sauti zao na hakuna ya yote angetambua ilikuwa nini. . . Yohana alijua zilikuwa nini, lakini yeye alikatazwa kuandika habari zake. Yeye alisema, “Bali yule malaika wa saba, katika siku za kupiga baragumu yake, zile siri saba za zile Ngurumo Saba zitafunuliwa.” Na yule malaika wa saba ndiye mjumbe wa ule Wakati wa Saba wa Kanisa. Ona?

396. Je, unaamini kuwa wakati mmoja maskini Bibi-arusi anayeishi atakusanyika mahali fulani pamoja na kuwa na vitu vyote shirika, kama alivyofanya Bibi-arusi wa kwanza, labda kabla tu ya kule kuja kwa Bwana Yesu mawinguni?

⁷⁹ Sasa, waliniuliza kama naliamini. Siwezi kulithibitisha kwa Maandiko, ila labda wakati huo unakuja, labda, sijui. Huenda kukawa tu na... Mwaona? Kama utakuwako, ungetambulisha kukaribia kwa kurudi Kwake, ikiwa hivyo... Yeye alisema, "Lakini Yeye yuaja kama vile mwivi ajavyo usiku." Ona? yuaja ku... Kama kile kitabu nilichosoma kuhusu Juliet—Romeo na Juliet, Yeye yuaja ku—kumtwaa Bibi-arusi Wake usiku. Yeye atanyakuliwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua. Ona?

⁸⁰ Na nina shaka kama itakuwa hivyo, kwa sababu Biblia ilisema, "Wawili watakuwa kitandani; nitamtwaa mmoja na kumwacha mmoja; na wawili watakuwa kondeni; nitamtwaa mmoja na kumwacha mmoja." Ona? Kwa hivyo huenda wao... Kote ulimwenguni, hawatakusanyika mahali pamoja na kuwa na vitu shirika. Lakini makundi madogo yatakuwa yametawanyika kote duniani.

⁸¹ Naamini, labda Bwana akiruhusu, hili ni kundi ndogo lake. Labda kundi lingine ndogo kule Asia, moja kule Ujerumani, moja kule chini mahali penginepo. Nilipoona ono la yule Bibi-arusi hivi majuzi, lilikuwa la mataifa yote. Ona? Kwa hivyo Bibi-arusi hatakusanywa toka mahali pamoja, atakusanywa toka kote ulimwenguni. Na hilo hasa lathibitishwa na Neno, na Neno halijawahi kukosea kamwe. Na hata wa leo, maono hayajakosea kamwe, kwa sababu yamekuwa kulingana na Neno.

397. Je, kila aliye na ubatizo wa kweli na halisi wa Roho Mtakatifu wakati huu aweza kukosa kuwa katika kule kunyakuliwa kwa Bibi-arusi? Je, waweza kueleza? Twambie yale tunayoweza kukufanyia wewe kwa njia yo yote kuurahisisha mzigo. Sasa, si hilo ni nzuri. Ona?

⁸² La, hakuna lo lote mwezalo kufanya sasa hivi.

⁸³ Naam, waamini halisi waliobatizwa na Roho Mtakatifu watakuwa katika Bibi-arusi. Bila shaka, wameteuliwa na kuitwa. Wale wanawali waliolala hawakuwa na mafuta yo yote. Wale waliokuwa na mafuta waliingia, lakini wale...

⁸⁴ "Tufanyeje kukurahisishia mzigo?" Naam, Ndugu, Dada, ye yote yule anayeandika hili, niombe; hilo ndilo jambo nzuri mno kufanya. Asante. Sihitaji pesa. Ni... Hizo huja za kunisaidia. Nashukuru Mungu kwa ajili ya hilo. Sihitaji mavazi. Mara nyingi sana watu hunipa nguo zangu ninazovaa. Na marafiki zangu na kadhalika hunipa nguo. Nao... Mimi hupata pesa za kutosha kulisha jamaa yangu; hizo tu ndizo tunazohitaji. Yaonekana... Na mnaweza kuniombea haidhuru, kwa sababu hakika ninahitaji msaada wa kiroho.

398. Yaonekana kwamba kati ya wahudumu wa Neno, kuwa hatuna mzigo au uliopo ni mdogo sana wa kuomba, kuhubiri, kufunga, au kwa ajili ya nafsi zilizopotea ambazo huenda bado ziko nje mahali fulani ulimwenguni. Tafadhali tuambie tufanyeje kuhusu hali hii? Asante sana, Ndugu Branham, kwa ajili ya hili. Haina budi huyo ni mhudumu. Yeye hakuandika jina lo lote kwa maneno haya.

⁸⁵ Ndugu... Ilinibidi kuyajibu huku nimechoka, nimedhoofika, na nimekuwa, unajua, sijisikii vizuri sana, kwa hivyo ni—ninatumaini kuwa linajibu hilo swali. Ni—ninakushukuru sana na ni—nilisahau yale ningelimjibu.

⁸⁶ Wahubiri, wahudumu sababu gani tuna mizigo hii—na hatuna mizigo kwa ajili ya nafsi zilizopotea. Naamini kuwa ni—ni kukosekana kwa ufufuo. Naamini yatupasa tuendelee kujaribu kumwomba Mungu atupe hamu kwa ajili ya nafsi zilizopotea hata Yesu atakapokuja.

399. Ndugu Branham, unaamini kuwa kila mmoja aliye na Roho Mtakatifu hunena kwa lugha? (La!) Najua unasema kuwa kunena kwa lugha—kunena kwa lugha si ishara ya Roho Mtakatifu. Ninge... I Wakorintho 12:30, tafadhali fafania. Je, mwaweza kupata I Wakorintho 12:30? Nadhani, “Je, wote hunena kwa lugha,” na kadhalika; sina hakika. Nitajaribu kupata lingine wakati wanapolijibu.

400. Ndugu Branham, je waweza kufafanua Ayubu 14:21?

⁸⁷ Naam. Ayubu 14 ni, “Mtu akifa ataishi tena.” Ee, mtu akifa... Ayubu akinena kuhusu ufufuo (Nafikiri nilikuwa na hilo asubuhi iliyopita, sivyo? Au ilikuwa kule nyumbani kwa Charlie? Bi. Cox alikuwa kule mahali fulani)—Ayubu, yeye aliona jinsi maua hufa na kuishi tena, lakini yeye aliingia ardhini na hangerudi tena. Ndiposa alielezwa kuwa kitu fulani kilikuwa kimetenda dhambi. Yeye alihitaji mpatanishi kati yake na Mungu, kisha yeye akaona kule kuja kwa Bwana.

⁸⁸ Ni nini Ndugu? [Ndugu Branham aongea na ndugu—Mh.] Nadhani hilo lilikuwa I Wakorintho 12:30. Naam!

“Je, wote hunena kwa lugha?” Hivyo ndivyo nilidhani ilivyokuwa, lakini sikuwa na hakika, nikiwa mchovu hivi, lakini... La! Wote hawaneni kwa lugha, wote hawafasiri; wote hawasemi hivyo. Ndiposa sura inayofuata. “Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika na sina upendo, si kitu mimi.” Ona? Paulo, kwa maneno mengine, akiwaambia wao, “Je, wote wananena kwa lugha? Hakika, hawaneni. Je, wote wanatabiri? La. Bali takeni sana karama zilizo bora; hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora.” Ona? Wote hawaneni kwa lugha.

Je, utakuwa na ibada nyingine ya upambanuzi kabla hujaondoka? Kama sivyo, je inawezekana kupata mahojiano ya kibinafsi?

Natumai ulipata. Sasa, sina mengi sana. Hebu nijaribu kuyapata nikiweza.

401. Nakumbuka nilikusikia ukisimulia jinsi uliona tamasha ya kuhuzunisha ya malaika—ya tai akipiga mbawa zake tunduni, akijaribu kuwa huru. Nina mama mpendwa katika hali hiyo. Yeye hajaruhusiwa kutembelewa nyumbani na watoto wake watatu walioolewa kwa miaka mitatu, kwa sababu hawawezi kutii mafundisho ya baba yao. Yeye ni mhubiri wa kidhehebu. Mama ataka kusikiza huu Ujumbe wa wakati wa mwisho, nami hata siwezi kuandika barua ikamfikia. Yeye inampasa kutii umbali gani? Je, kuna lo lote niwezalo kufanya mbali na kuomba?

Hilo lingekuwa tu ndilo jambo nijualo. Mume wake, akiwa mhudumu, hawezi kumruhusu asikize Neno. Yeye ataka kulisikia, lakini huyu hawezi kumruhusu alisikie, basi mwombeeni tu. Naamini mwanamke huyo ame—ameokoka, bila shaka.

402. Ndugu Branham, je yawezekana kwa mtu kupotea na kuishia kuzimuni kama akikataa Nuru ya Neno, ijapokuwa ana tukio halisi la kuhesabiwa haki na kutakaswa?

⁸⁹ Naam, bwana! Ndivyo hasa.

403. Unapotumia usemi kwamba tusipoamini Neno, tutatengwa milele na Kristo, je, unamaanisha wale wanawali wapumbavu wataishi milele, ila watatengwa na ile Yerusalemu Mpya ambamo Kristo ataishi pamoja na Bibi-arusi? Hapa kuna wale ambao hawana Roho Mtakatifu, wamezaliwa mara ya pili kama Maandiko yasemavyo kuhusu kuzaliwa mara ya pili. Kama kuzaliwa kwa kawaida kunahitaji maji, damu, na roho, je, si kuzaliwa kwa kiroho kunahitaji viwango vyote vitatu vya neema kabla mtu hajazaliwa kweli mara ya pili?

⁹⁰ Hakika, nilieleza hayo asubuhi hii—vivyo hivyo, juu ya jambo lile lile. Yakubidi uwe na hatua hizo zote. Umezaliwa kwa Roho, kama tu mtoto mchanga anavyozaliwa katika tumbo la mama, lakini hawajazaliwa hadi wamepokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Umezaliwa wakati huo, hujaongoka bado. Uko njiani kuongoka hadi wakati huo.

⁹¹ Hiyo ndiyo sababu siri hizi sote hazingetolewa kwa Luther, hazingetolewa kwa Wesley, hazingetolewa kwa wakati ambao umekwisha pita karibu nasi, ule wakati wa Kipentekoste. Kwa nini? Wakati haukuwa umewadia. Walikuwa wamezaliwa. Naam, Utu wa Kristo, Mwenyewe, yule Mwana wa Adamu (mwafahamu?) akijifunua Mwenyewe katika mwili wa kibinadamu, haungelikuja hadi sasa.

404. Ule Utawala wa Miaka Elfu utakapoanza, wasioamini wataondolewaje duniani?

⁹² Wasioamini wataingia katika ule wakati wa ile dhiki pamoja na wale wanawali waliolala, na hao wengine wote (wasioamini, na wanawali waliolala), na wazao wa Israeli waliosalia watakaotwaliwa.

405. Ndugu Branham, wakati baadhi ya—mtu fulani anaponiudhi au “kukanyaga vidole vyangu (Huenda hili likawa zuri.)—kukanyaga vidole vyangu,” kama msemu wa kale ulivyo, ninaingiwa na hasira; nawezaje kushinda jambo hili? Najua Bwana atapaswa kufanya hivyo, lakini nifanyeje moyoni mwangu? Sitaki kitu hiki.

⁹³ Tia utamu hasira yako kwa maombi, kisha ujiazimie. Hamna... Sidhani kuna watu wengi sana jengoni humu waliopata kuwa na hasira kali kama nilivyokuwa nayo mwanzoni. Lo, m—mdomo wangu uliponda-pondwa kila wakati. Nami—ni—ningekula baadhi ya vyakula vyangu kwa mrija.

⁹⁴ Mama yangu, kama mjuavyo, alikuwa nusu Mhindi, na baba yangu alikuwa M-Irishi, M-Irishi halisi wa Kentucky. Na kila mmoja wao alikuwa na hasira ya kutosha kupigana na msumeno uvumao. Na wakati wote mdomo wangu ulikuwa umeponda-pondwa; kwanza nilikuwa mdogo. Nao wangeninua tu na kunitupa chini. Nami ningeamka tena; nao wangenitupa chini tena hadi nilipoweza sana—singeweza kuamka tena. Hiyo ilikuwa kila mara. Ndiposa nilipoweza kuamka, niliamka tena; wakaniangusha chini tena. Kwa hivyo hivyo ndivyo ilivyotendeka kwangu.

⁹⁵ Niliwazia, “Siwezi kamwe kuwa Mkristo.” Lakini Roho Mtakatifu alipoingia maishani mwangu, hiyo ilikwisha. Hamna tena...

⁹⁶ Nilikuwa na mwanamke wakati mmoja; nilienda kukata stima. Na siku hizo nilikuwa na nywele kichwa mwangu. Yeye alisema, “Ewe maskini mbilikimo, baradhuli kichwa-maji!”

Nilimwambia, nikasema, “Mama, hupaswi kunilaani hivyo. Jamani, humwogopi Mungu?”

Yeye alisema, “Ewe maskini mbilikimo, baradhuli kichwa-maji, kama nilitaka mtu fulani aongee nami kuhusu mambo kama hayo, singempata mtu mjinga kama wewe.”

“Wuuu!” Ndipo yeye *akanikashifu*, akaniita majina ya *kukashifu*. Jamani, kama ingekuwa mwaka mmoja hapa kabla! Mimi kila mara nilisema, “Mwanamume ambaye angempiga mwanamke hakuwa mwanamume kutosha kumpiga mwanamume,” lakini hu—huenda ningevunja hilo wakati huo kwa kumwita mama yangu jina kama hilo. Lakini mwajuaje? Hata haikunidhuru. Nilisema, “Nitakuombea.” Haikuniudhi... Nilijua wakati huo huo kitu fulani kimetendeka kwangu. Naam, bwana! Jamani!

⁹⁷ Mwajua maovu niliyoyafanya nilipokuwa mdogo, kupigana! Karibu niue watu watano wakati mmoja. Nilichukua bunduki iliyokuwa na risasa kumi na sita, na wavulana wale waliponipiga kwa sababu nilikuwa Mkentucky, hakuna sababu nyingine... Hata singekiinua kichwa changu. Mmoja angenishika mikono hivi, na mwingine angesimama pale na jiwe mkononi mwake na kuniponda usoni, hadi sikujifahamu. Hakuna cho chote kamwe...

⁹⁸ Waliniita, "Chotara wa Kentucky," kwa sababu mama yangu, yeye alipokuwa msichana, hakika alionekana kama Mhindi (Nilipotazama picha yake muda mfupi uliopita), nao walijua yeye alikuwa nusu Mhindi. Na kwa sababu nilikuwa Mkentucky naye akiwa mwanamke Mhindi, waliniita mimi "chotara, chotara wa Kentucky." Na halikunihusu kwa vyo vyote vile; singejizua kuzaliwa Kentucky.

⁹⁹ Nilienda kule chini shuleni, nami sikuwa na mavazi ya kuvalia, na nywele zangu zikipepea chini ya shingo langu. Na Baba—Mama alichukua koti kuukuu Baba alilovaa alipooa, na kulikata na kunitengenezea suruali fupi mbili nivalie nikienda shuleni mara ya kwanza. Nami...Naye alinivalisha jozi la soksi mbili nyeupe na jozi la viatu vya raba. Nao walisema, "Kama huonekani kama "Mkentucky-ovyo." Na—na yote—na hayo—ndiposa, hilo liliendelea siku zangu zote—siku zangu zote shuleni.

¹⁰⁰ Na wavulana kadha, kwa sababu nilitembea njiani na msichana mdogo na kubeba vitabu vyake...Hawakunitaka mimi nifanye hivyo, nao walinikabili kule chini na kunipiga hata nikazirai. Niliwaambia, kama wangepigilia tu niende, naahidi kuwa ningeenda moja kwa moja nyumbani. Na kwa hivyo wao wakachukua—wakaniachilia, wakanipiga mateke mara nne au tano, wakaniangusha chini, na kupwaruza uso wangu wote. Nami nilienda nyumbani, hivi, kupitia vichakani.

¹⁰¹ Nilikuwa na bunduki muundo wa .22 Winchester imewekwa juu ya mlango. Nikaichukua na kuijaza hiyo bunduki risasi, nikapitia kichakani mwa nzige na kujificha kando ya njia hata wavulana hawa watano au sita wapitie pale. Nilingoja tu hata walipokuja, na ndipo walipokuwa wakija pale, wakiongea, kasema, "Huyo Mkentucky atatambua aliko tangu leo," wakiendelea hivyo.

¹⁰² Nilijitokeza huku nimevuta mtambo wa ile bunduki. Nikasema, "Sasa, nani kati yenu anayetaka kufa kwanza, ili asiwaone wengine?" Walianza kulia; nilisema, "Msilie, kwani ninyi nyote mtakufa mmoja baada ya mwingine." Nami nililikusudia! Na papo hapo walianza kulia. Nami nilivuta mtambo wa bunduki na kufyatua! Bunduki ilifyatuka. Niliingiza risasi nyingine. Kafyatua, ikafyatuka; risasi nyingine, kafyatua, ikafyatuka. Nami nilitupa risasi kumi na sita ardhini.

Kila moja ilifyatuka. Na wavulana wale wakikimbia, na kulia, na kwenda kifichifichi kule mlimani, na kadhalika.

¹⁰³ Nao walipoondoka, nilisimama pale. Iwapo nilipata kukasirika sana, hata si—si—singelia, ningecheka kama baradhuli na machonzi yakidondoka machoni mwangu. Sasa, hiyo ni hasira. Kama haingekuwa Mungu, ningalikuwa muuaji.

¹⁰⁴ Nami niliokota risasi zile kuzirudisha tena katika bunduki, na, “Pooou, pooou”; zingepiga tu kama hapo mbeleni. Nena kuhusu neema!

406. Wako wapi wale wanawali wapumbavu wakati wa ule Utawala wa Miaka Elfu?

¹⁰⁵ Katika ule Utawala wa Miaka Elfu wao wako kaburini. “Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, kwa miaka elfu.”

407. Kutakuwako, au sasa kuna mahali pa Bibi-arusi kukusanyikia na kuishi, kama wakati Musa alipowaongoza wana wa Israeli?

¹⁰⁶ Nitawajibu swali hilo; ilifunuliwa kwangu hivi majuzi. Nitawaambieni kweli. Naam, bwana! Kuna mahali watakapokusanyika Bibi-arusi wote. Mnataka kujua ni wapi? Katika Kristo. Hakika. Kusanyikeni tu ndani mle; sisi sote tuko pamoja.

408. Sababu gani tunafanya mzozo mkuu kuhusu mavazi ya wanawake (Ee, ee, nitajutia hili, sivyo?)—mzozo mkuu kuhusu mavazi ya wanawake, kukata na nywele na—hamna lo lote linalosemwa kuhusu nywele za wanaume au jinsi yeye avavyo?

¹⁰⁷ Vema, Dada, nitakubaliana na wewe kwa jambo moja. Kwanza, Biblia ilisema kuwa mwanamume hapaswi kuwa na nywele ndefu. Na kama angekuwa na nywele ndefu, ningemwambia, kama tu nikwambiavyo wewe. Yeye amekosea. Lakini wanaume wengi, wengi wao kama mimi, hawana nywele kamwe. Lakini wanaume wengi hukata nywele zao, huonekana kama wanaume. Na sasa, kama hawakufanya hivyo, wangelambiwa wasifanye hivyo, kuachilia nywele zao zikue kama nywele za wanawake. Nyote mtapata haya yote katika nadhiri za ndoa na talaka na kadhalika tutakapozihubiri. Mzozo mkuu kama mavazi ya mwanamume—au mavazi ya mwanamke...

¹⁰⁸ Sasa, mwanamume, kwanza mwili wa mwanamume si wa kutamanisha kama wa mwanamke. Sasa, mwanamume, yeye ni mnene, mzee, miguu yenye malaika, mwenye vigosho, mwenye tumbo kubwa, na kadhalika, yeye anaonekana kitu cha kuchukiza sana; na hana cho chote cha kutamanisha. Nami nadhani inaonekana jambo la “kuchukiza mno” kuona wanaume hawa wakitembea barabarani, vijana kwa wazee, wamevalia hizi suruali fupi, sijui mnaziitaje, mwajua, wakitembea barabarani.

Nadhani hicho ndicho kitu kichafu mno nilichopata kuona. Hiyo ni kweli. Nafikiri ha—hajui yeye ni wa jamii gani (ona? Naam!), mwanamume ambaye angefanya jambo kama hilo.

¹⁰⁹ Nanyi mwajua? Nilisikia tu miezi michache iliyopita, Jeshi la Amerika litavalia hivyo. Naam! Jeshi litakalofuzu mwaka ujao, au baada ya mwaka ujao, wote watavalia suruali fupi. Twaweza kupata kundi kubwa vipi la kijike?

¹¹⁰ Mungu alimwumba mwanamume aonekane kama mwanamume, na atende kiume, na avalie kiume. Yeye alimuumba mwanamke awe vivyo hivyo, avalie kike, atende kike, awe wa kike. Kuhusu asubuhi hii—kuhusu—swali lilizuka kuhusu wanaume. . . [Upande wa kwanza wa kanda unakwisha bila kukamilika na upande wa pili unaanza bila kukamilika—Mh.] Yeye akitaka ku. . .

¹¹¹ Kama mwanamke ana nywele fupi sana, naye ataka moja ya hivyo “vipanya.” Ni. . . Mke wangu huvivalia. Ni. . . Yeye husema nywele zake ni haba naye ana kitu kama duara kubwa hivyo, chaonekana kama biskuti kubwa, kubwa mno. Naye hufungia nywele zake kukizunguka na kuzishikilia kwa visindano. Na sasa, ile kwangu mimi, hilo—hilo haliudhi cho chote mradi tu nywele zako ni ndefu.

¹¹² Mhudumu fulani alisema mke wake alikuwa—alihukumiwa, kwa sababu yeye alikuwa na—na wanja nyweleni. Nami nilitambua kwa swali, hilo maana yake ni rangi au kupaka rangi nywele zake. Siwezi kusema hilo ni kosa; sina neno kuhusu hilo. Mradi tu ana nywele ndefu, hilo tu ndilo niwezalo kusema kuhusu hilo.

¹¹³ Na sasa, mwanamume. . . Mtu huyu alisema asubuhi hii akitoa nywele zake, na kuzivalia. Sasa, hili lilifika hapa, kuhusu kunyoa nywele. Ona?

¹¹⁴ Sasa, kama—kama mwanamume hana nywele, na mkewe. . . Nimesikia wanawake wakisema, “Vema, kama ningemfanya tu Yohana. . . Nadhani angeonekana bora kama yeye ange—angevalia nywele bandia. Waonaje, Ndugu Branham? Ni kosa kwake kufanya hivyo?” La, bwana! La, hakika, si kosa, kwa vyo vyote vile. Kama yeye ataka kuzilivalia, sawa, si zaidi ya kutia meno bandia au cho chote kile.

¹¹⁵ Walakini, mimi mwenyewe nina meno matatu bandia. Laiti nisingalikuwa nayo. Yako kwenye waya; kila mara hupweza sauti yangu, na kukata ulimi wangu, na kadhalika, lakini yanipasa kuwa nayo nipate kula. Na kama nina. . . Ninapokuwa kule ng’ambo kwa mojawapo wa mikutano ya nje, mimi huvaa nywele bandia; si kwa sababu ya kuonekana kwayo, kwa sababu mwajua ningesimama papa hata hapa kama singekuwa na nywele kichwani mwangu au cho chote kile. Halingenifanya tofauti hata kidogo; mimi niko hapa kumwakilisha Yesu Kristo. Lakini nisimamapo nje pale, yapata usiku wa kwanza katika

hizo tufani za tropiki, usiku unaofuata koo langu limekauka mno siwezi kwenda nje kule.

¹¹⁶ Kwa hivyo basi, kama—kama mna jambo fulani nililotaka kufanya, na kuonelea nilifanye, ningelifanya. Naam, bwana! Hakuna kitu kinachosema usilifanye. Hakuna kitu kinachosema, Dada, kuwa huwezi kuvaa nywele bandia au mwengo wa nywele, au kitu kama hicho katika . . . Hilo ni sawa kabisa, lakini acha nywele zako ziwe ndefu. Nawe mwanaume, kata zako. Ulizo nazo, hebu ziache. Ona? Basi hilo latosheleza.

¹¹⁷ Nawe mwanamke, valia kike. Nawe mwanamume, valia kiume; msijaribu kuwa wa kike na kuvaa mavazi ya wanawake. Nanyi wanawake, msijaribu kuwa wanaume na kuvalia kiume, kwa sababu Mungu hawataki mfanye hivyo; Biblia inakataa jambo hilo.

¹¹⁸ Lakini sasa, kuhusu kuvaa nywele bandia au kuvaa unywele . . . Vema, nini mojawapo wa hivyo “vipanya”? Je, nilikosea muda mchache uliopita au hilo ni “panya mdogo”? Ni—ni kitu fulani—ni kitu ambacho mwa—mwanamke huweka katika nywele zake kuzifanya zionekane nyingi . . . Sijui kinaitwaje (ona?), hakuna ubaya kwake. Endelea, ni sawa.

409. Ndugu Branham, dada fulani alikuja humu maskanini toka maili mia nane, naye alisema aliamini wewe ni Yesu Kristo aliyechukua umbo la mwanadamu. Tafadhali eleza hili. Yeye hakuwa na (s-a-b-u—) saburi hata kidogo katika kuwaeleza wengine yale anayowazia, hakuwa na (s-a-b-u-r-) saburi . . . Vema.

¹¹⁹ Sasa, bila shaka dada yule alikosea. Mimi si Yesu Kristo; Mimi ni mtumishi Wake. Tumeeleza hayo mara nyingi sana. Lakini . . .

Ee, niko karibu sana; sasa; niombeeni, muda mdogo sana.

410. Ndugu Branham . . . (Mngependa tu kusikia mengine yayo u—upesi niwezavyo?) Ndugu Branham, wakati mmoja nilishindwa Mungu alinipa — najisikia Mungu alinipa ahadi kama ya Sara. Kulikuwa na swali, lakini ahadi ilikuja baadaye. Je, hiyo ahadi ilikuwa ya Mungu? Najua ya Sara ilikuwa vile, lakini naona wakati ni mfupi sana. Tunapenda huduma yako na Yeye aliyekuita (Hilo ni zuri, sivyo?)—tunapenda huduma yako na Yeye aliyekuitia hiyo, na kwa hivyo, tunakupenda. Ee, waliandika jina lao. Asante, Dada na Ndugu. Swali, naam, naam. Vema.

¹²⁰ Sasa, Mungu . . . Nafikiri Yeye aliwapa hiyo ahadi, na ilitendeka kama Sara. Hakika, ni Mungu yule yule; Yeye hujibu vivyo hivyo. Msiamini lingine lo lote ila kuwa ilikuwa ya Mungu.

Ndugu Branham, ningetaka kukuuliza maswali kadha kuhusu Biblia. Tafadhali fafanua Marko Mt. . . .

Nimefanya hivyo; nimefanya hivyo, Marko Mt. 16. Tulifafanua hilo hivi majuzi, nakumbuka. Hebu tuone.

411. Mpendwa Ndugu Branham, tafadhali fafanua Mathayo Mt. sura ya 22, kifungu, wakati...(Tulifafanua hilo. Ona? Mnakumbuka hivi majuzi? Nita—nitawaonyesheni. Nilikuwa...Mnaliona papa hapa?) **22...Mgeni huyu aliingiaje katika ile Karamu ya Arusi, ambaye hakuwa na lile vazi, lakini hakuwa na mojawapo wa yale mavazi ya arusi?**

¹²¹ Kumbukeni, nilisema...Nilifanya mzaha mdogo; nilisema, “Ndugu wa kidhehebu aliingilia di—di—aliingilia dirishani na si kupitia kwa Mlango.” Mlango ule ni Neno.

Ulisema Kaini alikuwa mzao wa nyoka. Mbona hawa alisema, “Nimempata mtoto mwanamume kwa Bwana?”

Hilo ndilo nililokuwa najaribu kulipata asubuhi hii. Nina Maandiko niliyoyaandika hapa kwa ajili ya hilo. Huenda nikaeleza hilo zaidi; natumaini. Kupata mengine hapa...

Ndugu Branham, mume wangu, aliyekuzwa Mkatoliki katika ibada zetu, yeye ataka kuomba atakavyo...

Nilijibu hilo. Mnakumbuka?

Ee, napata haya papa hapa sasa. Nilijibu hilo.

Ndugu Branham, mimi mwishowe...kumshawishi dada yangu atoke kwa dhe—nilijibu hilo. Huyu mwanamke alikuwa na dada mkatoliki.

Ndugu Branham, katika 2 Timotheo 4 ni karama gani aliyopewa kwa...

Nilijibu hilo. Wangapi wanayakumbuka? Nimeyachangayisha mengine juu hapa. Ona?

Ni halali kwetu kutumia aina yo yote ya...

¹²² Hilo ni kupanga uzazi. Ni—ni...Hebu niongee nanyi kwenye—kwenye mahojiano ya kibinafsi kuhusu hilo (ona?), kama nilivyosema asubuhi hii.

Kwanza, je, wale wanawali watano wataokoka katika ule...

Nilipata hilo. Narudia hapa. Hebu kidogo, nisubirini.

Baada ya kujua, njia iwayo yote ya toba na kutakaswa (Nilijibu hilo, mwakumbuka), ndipo wakaanguka toka kwa hiyo...

Nilijibu hilo pia. Nimeyarudia kidogo. Yanipasa tu niyapate kama...

Ndugu Branham, nini maana ya Mathayo Mtakatifu 24:28, “Kwa kuwa po pote ulipo mzoga, ndipo watakapokusanyika tai?”

Mwakumbuka nilieleza hayo? Ona? Niliyajibu. Labda nimeyamaliza. Bwana asifiwe!

Ni wakati—je, wakati umewadia ambapo Bibi-arusi atapaswa ku—kuwa pamoja nawe kwa ajili (sasa, nilipata hilo.) kule kunyakuliwa?

Labda mimi...Nami najua nilijibu hilo, kwa sababu lilikuwa limetiwa alama hapa chini; nakumbuka hilo. Vema, Bwana, asifiwe! Tunafikia chini hapa sasa. Hebu tuone.

412. Kwa kuwa Matendo 2:38 ndiyo njia pekee ya kubatizwa, vipi kuhusu ule umati...? Nilijibu hilo.

¹²³ Hawakulijua katika siku zao; limefunuliwa tu sasa. Baada ya kujua la kufanya, “Basi yeye ajuaye kutenda mema wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi.”

413. Ndugu Branham, je ni kosa kupanda—kupanda na kufanya kazi ya tumbako? Siamini nilijibu hilo.

¹²⁴ Sasa, nachukia tumbako. Nachukia matumizi ya tumbako; Mkristo ye yote aliyezaliwa mara ya pili ataichukia; hivyo tu, kwa sababu ni kosa. Twajua hata sayansi ya madawa inasema hiyo ndiyo huanzisha sana ugonjwa wa kansa ya Koromeo na—na ya mapafu, ni—ni tumbako. Wao husema, “Vuta sigara zenye chujio.”

¹²⁵ Sasa, kwenu wanaume na wanawake mnaovuta sigara, hilo linawadanganya ninyi tu, kwa sababu hamwezi... Vema, jambo pekee wanalofanya... Mnaponunua sigara zenye vichuji, hamna budi kununua nyingi zaidi, kwa sababu zinaruhusu tu kadiri fulani ya moshi upite. Kwa sababu mtu ye yote atakwambia...

¹²⁶ Nilisikia hiyo hotuba kwenye Maonyesho ya Ulimwenguni kule Washington mwaka uliopita (nilipokuwa kule katika Maonyesho ya Ulimwenguni) na hao madaktari toka ulimwenguni kote pale walilieleza; kasema kwamba huwezi kupata moshi bila lami, na huwezi... Na kama una moshi una lami. Kisha kasema, “Mtu ye yote asikudanganye kwa sigara zenye vichujio, maana ambapo ungevuta moja au nyingine ambayo ingeridhisha tamaa uliyo nayo kwa sigara, utavuta mbili au tatu za zile zingine.” Ni kutuliza tu u—umma, kunyamazisha uenezaji habari kwenye redio na televisheni.

¹²⁷ Lakini kufanya kazi kwa tumbako au kuikuza. Sasa, ninyi ndugu wa Kentucky mnaokuza hii tumbako... Vema, hebu niseme jambo moja: Kama linakuhukumu wewe kufanya hilo, usilifanye, kwa sababu singependa kufanya lo lote ambalo linge—ambalo najua linamwelekeza mtu mwingine katika mauti. Ni kosa kumpa jirani yako pombe, basi ingekuwa kosa kupika pombe. Lakini hebu niseme jambo lingine sasa. Sasa, kuhusu kuikuza...

¹²⁸ Tumbako, mwajua, sumu iliyo katika tumbako hutumika pia katika madawa. Basi je, mlifua mnakuza mahindi yanayotumiwa

kutengenezea whisky, ngano na shayiri vinavyotengenezea whisky? Sivyo? Vema. Ona? Hamjui wataitumia kwa nini.

¹²⁹ Lakini sasa, tunakuza mahindi, ambayo twaweza kuwazia tunapokuza mahindi, kuwa huenda ikatumiwa kwa biskuti, na chakula kwa watu, ugali, na vinginevyo; lakini wao pia hutengenezea vinywaji vya kulevywa kwake (ona?), kwa hivyo hungejua la kufanya.

¹³⁰ Na unakuza—una nyinyoro bustanini. Mnajua wanafanyia nini nyinyoro? Wanatengeneza kasumba kwake. Mwajua wanafanyia nini saladi? Kitu kile kile. Kasumba pia iko katika saladi. Je, uliwahi kula saladi na kuona jinsi unavyojisikia mtulivu kwa muda mchache? Ni kasumba iliyomo. Je, mwajua imo katika vitunguu? Bila shaka. Kwa hivyo, mwa—mwaona, inategemea unaifanyia nini.

¹³¹ Lakini hebu niseme hili kama ndugu Mkristo kwa ndugu Mkristo; Kama una shamba la tumbako, uzia mtu mwingine na ujaribu kukuza mahindi badala yake. Naamini ingekuwa heri (ona?), kwa sababu si shaka kile wanachoikuzia hiyo . . .

Mume wangu alioa mlevi na mzinzi . . .

Nilijibu hilo. Latoka . . . Niliwaambia lilitoka. Limetoka mbali na hapa. Nilijibu swali hilo. Na sasa, hebu tuone.

Yule mwanamke wa Ufunuo 12 . . .

Nilijibu hilo. Naam, nimejibu kundi hili la maswali. Hebu tuone. Yanayo; nimeyajibu. Iko katika Ufunuo 12, jinsi alivyokuwa. Hebu tuone.

414. Ndugu Branham, tuna watoto wawili wanaoenda kanisani linalosimamiwa na mhubiri mwanamke. Tunajua yeye yuko nje ya Neno. Watoto wetu wako chini ya huu ushawishi mkuu. Tutafanyaje kuwaambia hili ni kosa?

¹³² Niliwaambia hapo awali. Nilijibu hilo. Basi lishughulikie pole pole. Utasemaje kama nili . . . najua mtu huyo anaketi hapa. Unasemaje kama naamini najua mwanamke huyo ni nani na naweza kukwambia?

415. Je, ule Utawala wa Miaka Elfu utakuwa miaka elfu au muda fulani tu wa wakati?

¹³³ Nilijibu hili asubuhi hii. Ona? Ni miaka elfu. Vema.

Ndugu Branham, shida ya yale . . .

Naam, nilijibu hilo. Ngano na magugu, mwakumbuka tulijibu hilo.

Naamini tunaelekea chini sasa. Huenda nilirudisha kundi la haya humu. Hebu tuone. Jambo lile lile.

Ndugu Branham, mimi ni mama wa watoto sita wapendwa na mume wangu anataka niende nifanye kazi kidogo nisaidie kwa pesa. Niende? Pia nataka kumwomba Mungu anipe imani—kunipa . . . Ibrahimu na—na kama imani—

ama Ibrahimu na Danieli na wale wana Waebrania. Je, Mkristo aweza kukuza tumbako? Nilijibu tu hilo na . . .

416. Ndugu Branham, Je ni kosa kwa mwanamke kunyoa miguu yake?

¹³⁴ Je, naona mambo? Je, hilo lasema hayo? Siwezi. . . Sijui. Nitakuachia wewe hilo.

Je, si—siku hizi ni kosa kupanga jamaa yako? Je, ilimaanisha kupanga uzazi kabisa?

¹³⁵ Nilijibu hilo bila shaka kwa—kila mtu binafsi. Hebu tuone.

Kama mwanamke hali akiwa katika dhambi anatalikiwa na kuolewa tena na . . .

¹³⁶ Nilijibu hilo. Mwakumbuka nilisema, “Acheni mambo ya talaka hata. . .”

417. Nina rafiki wa kike ninayempenda sana. Amekuwa na kanda na barua ambazo naamini zime . . . sijawahi kuongea naye. Hakika, nafikiri naogopa kumharibu na kumpoteza kama rafiki. Nifanyeje?

¹³⁷ Ongea naye katika upendo. Mimi si-. . . Naamini nilijibu hilo, lakini si—mimi si—usijaribu kumsukumiza cho chote kwa mtu ye yote. Kolea tu; watatamani kuwa kama wewe.

Ndugu, Dada, naamini nimejibu haya.

Ndugu Branham, tafadhali fafania kuhusu wale wanawali watano wapumbavu.

Ni—ninajua nilijibu hilo. Limeandikwa, na ni karatasi nyekundu. Naamini tuna-. . . Nilijibu hilo. Naamini nimejibu haya yote. Bwana asifiwe. Hebu tuone. Kunradhi tu kidogo.

418. Mpendwa nabii wa Mungu, Injili ya Marko 16:18, ni . . . sehemu ya kuweka mikono juu ya wagonjwa . . . mimi ni jirani ya washika nyoka. Vipi hao nao?

¹³⁸ Vema, hilo ni swali nzuri. Kama wewe ni jirani wa washika nyoka, nao walisema Marko 16. . . Bila shaka! Naamini Biblia inakusudia tu yale isemayo. Naamini tukijaribu kumjaribu Bwana katika jambo fulani, tutajuta. Lakini sidhani Mungu akusudia wewe uniletee chupa ya sumu kali kuona kama ningekunywa ili kuwathibitishieni kuwa nina imani, si zaidi ya ninavyoamini ingekuwa vema kwako kuniletea nyoka, na uache niishike, na kukuonyesha nina imani kuwa naweza kushinda sumu yake. Siamini hilo ni kweli.

¹³⁹ Naamini kuwa kama nilikuwa majini nikibatiza watu, au kufanya kazi ya Bwana, au kule porini, na nyoka aniume, ningeendelea kutembea tu katika Jina la Bwana. Ona? Naamini kuwa hilo ndilo ililomaanisha.

¹⁴⁰ Sasa, kama yakupasa kushika. . . Ona, cho chote ufanyacho kwake, mtu mpendwa ye yote yule—sijui wewe ni nani. . . Kumbuka hili. Ona? Chunguza yale Biblia ilifanya kuhusu hilo.

Si zaidi kuliko ninavyoamini kuwa kama ukijaribu kusema, “Utukufu, utukufu, utukufu” . . . Usimjaribu Mungu kunena kwa lugha, acha tu Roho anene kupitia kwako. Ona?

¹⁴¹ Sasa, siamini katika kumjaribu Mungu au kusukumizia lo lote. Kama tu nilivyosema muda mchache uliopita, Roho anapo . . . Tunamngoja Roho; anafanya.

¹⁴² Sasa tazama, Paulo alikuwa akikusanya kuni kwenye kile kisiwa cha Krete; naamini ilikuwa kule. Naye alikuwa katika minyororo, na nyoka, labda mamba . . . Huko ni kuuma kwa mauti; ilimpasa kuanguka mara moja, maiti. Sijui nyoka mwingine ambaye angeua upesi hivyo, isipokuwa awe mamba.

¹⁴³ Na kwa hivyo yeye alimwinua huyu mamba, tuseme. Ni kuuma kwa mauti; umebakiza tu, ni kupumua kidogo tu kulikobaki. Mamba anapokuwa . . . Au swila, una nafasi hamsini kwa hamsini kwa ute huo kuishi—ukiumwa na swila mweusi. Na swila wa manjano ana kifo cha asilimia themanini na asilimia ishirini kuishi; halafu kwa mamba, hauna nafasi yo yote. Umekufa tu, hivyo tu, kwa sababu hupumui ila tu pumzi chache. Inapooza mishipa ya fahamu, mwenendo wa damu, na kadhalika, nawe umekwisha. Ona?

¹⁴⁴ Lakini wakati—huyu mamba alipomuuma Paulo mkononi, wao walisema, “Vema, mtu yule ata—yeye ni mtu mwovu, labda muuaji. Ijapokuwa aliepuka baharini, bali ile—yeye hangeepuka kifo. Miungu itajilipizia kisasi hivi—kwa kuwa yeye ni muuaji.”

¹⁴⁵ Paulo alitazama, huku huyu nyoka akining’inia mkononi mwake, yeye alimtikisa akaanguka, bila kupiga mayowe, “Ee, Bwana, nisaidie nifanye hivyo.” La! Yeye alimtazama, akamtikisia motoni, akaendelea kukusanya kuni kama kwamba hakuna cho chote kimetendeka.

Wao walisema, “Yeye atakufa katika dakika moja hivi, kwa sababu mara nyoka huyo akuumapo, umekwisha.” Baada ya muda mchache kupita, Paulo hakuvimba, hakufa, wala kupatwa na dhara. Wao walisema—wakageuka, wakasema, “Yeye ni mungu aliyeshuka katika mfano wa mwanadamu.” Ona?

¹⁴⁶ Yeye hakusema kamwe, “Nileteeni huyo nyoka,” bali nyoka alimuuma. Yeye hakumjaribu Mungu kamwe, lakini alikuwa na imani kwa Mungu kushinda kule kuumwa na nyoka. Mwaona ninalokusudia?

¹⁴⁷ Kwa hivyo ye yote uliye kati ya washika nyoka, ni . . . Sasa, kama wanataka kushika nyoka, hilo—hilo ni juu yao. Ona? Silioni hivyo.

¹⁴⁸ Sasa, unasema, “Vema, hao watu wana imani.” Sisemi hawana imani, wanajichoma wenyewe na tochi ya hewa na mambo kama hayo, lakini (mwaona?) bado hilo halimthibitishi Mungu.

¹⁴⁹ Nimewaona Wahindi wakichukua m—mstari wa moto, wenye upana wa futi tatu na urefu wa yadi arobaini, wakati umepepewa sana kwa majani hata ukawa mweupe kwa joto (si watu maalum, wakulima), wanavua viatu vyao, wanachukua visindano (makasisi wanawabariki kwa damu ya mbuzi)—na kuchukua visindano vidogo vya ndoana, na kuvipenyeza ngozini mwao juu ya vinywa vyao, hadi wao ni farakano moja kubwa la—la maji, wamejaa kama mipira ya mti wa Krismasi hivyo, mapambo, yamejazwa, na ndoano kubwa urefu huu zimeshindiliwa mwilini mwao (ungewaza hizo ni nini kuchoma na kuchomoa), na kusimama hivyo, na kutembea moja kwa moja kupitia kwa ule moto mkali (na ni—ni mweupe kwa joto, umepita mwekundu, mweupe kwa joto)—wakitembea kupitia kwa huo moto na kugeuka na kurudi tena, pasipo hata kuungua miguuni mwao. Nao hata hawamwamini Mungu wetu. Huabudu—ibada za pepo. Ona? Kwa hivyo hilo halimaanishi kitu. Liondokee. . . Wewe kuwa tu Mkristo halisi, mwema, mnyenyekevu, uishi maisha hayo, kisha Mungu atashughulikia yaliyosalia.

419. Ndugu Branham, wahubiri watahubiri nini—watahubiri nini wale wasiokwenda pamoja na Bibi-arusi? Ujumbe wao sasa, Roho Mtakatifu, ubatizo wa maji, na wokovu, watahubiri nini wasipoingia katika Bibi-arusi?

¹⁵⁰ Vema, mwajua—mwajua kipi labda kitatendeka? Nasema hili, sasa. Siwezi kuthibitisha hili, lakini ni—wataendelea tu moja kwa moja kuhubiri kama wanavyofanya sasa, na watu wakiendelea kufikiria wao wanaokoka; naye Bibi-arusi atakuwa amekwisha uondok.

420. Ni sawa, kulingana na Neno kupanga uzazi?

¹⁵¹ Niliwaambia ninyi ningejibu hilo kibinafsi. Ninyi mlio na maswali haya, njooni peke yenu.

Mpendwa Ndugu Branham, tuna mwalimu ambaye unamjua ambaye Maandiko yasema. . .

Naam, nilijibu hilo. Hebu kidogo sasa.

Ndugu Branham, wakati mmoja majina yetu yaliandikwa katika kitabu cha. . .

Naam, nilipata hilo. Juu ya vile wao wameshaliondoa sasa, walifanya kosa?

421. Je—je, unaunga mkono upangaji wa uzazi?

¹⁵² La, siwezi kuuunga mkono. La, bwana! Ona?

422. Yule—je, yule malaika wa saba, kama alivyonenwa, wa Ufunuo 10, mtu mmoja na Eliya wa Malaki 4?

Je, nilijibu hilo? Hilo halionekani kama nililijibu.

¹⁵³ Naam, ni mtu yule yule. Ufunuo 10 ni Ujumbe wa malaika wa saba, ambaye—malaika aliye mjumbe wa saba wa Wakati wa Saba wa Kanisa, ambaye ni Malaki 4.

Je, kupanga uzazi . . .

¹⁵⁴ Ninayo mengi kama hayo. Niliyarudisha tu haya nyuma, nami sikutaka kuyajibu; heri niwaone ninyi faraghani.

423. Tunapata wapi ambapo Nuhu alihubiri kwa miaka 120 na kujenga safina katika miaka 120?

Je, nilijibu hilo?

¹⁵⁵ Kizazi, au wakati uliowekwa, muda uliokusudiwa kwa mwanadamu duniani ulikuwa miaka 120, ambao ulimchukua Nuhu, muda huo, kujenga safina, ambao ulihesabiwa kuwa kizazi kimoja siku hizo. Miaka mia moja na ishirini ulikuwa wakati aliopewa mwanadamu. Naye alihubiri, kulingana . . . Mwanzo 6:3, yeye alihubiria kizazi kile, ambacho kilikuwa miaka 120; Nuhu alifanya hivyo. Vema. Hebu tuone sasa.

424. Katika Malaki 4, huyu Eliya atachukua mioyo ya watoto kuwaelekezea baba, halafu mioyo ya watoto kuwaelekezea baba zao. Je, huyu ni mtu yule yule?

¹⁵⁶ Naam, mtu yule yule. Vema. Ee, ngoja kidogo. La! Samahani, nasikitika. Tu . . . Mnaona Roho Mtakatifu alinishikia mimi hilo wakati huo? La! Nilidhani ilisema ile . . . Ona?

¹⁵⁷ Jinsi ilivyokuwa katika Malaki 3, pale, “Angalieni, namtuma mjumbe wangu mbele Yangu,” ambaye alikuwa Eliya. Katika Malaki 4 inageuka na kusema, “Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii.” Malaki 3, Yeye angemchukua mjumbe aliyetumwa mbele za Bwana Yesu, ambaye alikuwa Yohana. Wangapi wafahamu hayo? Malaki 4, huyu Eliya ajapo, mara tu baada ya hayo—Ujumbe wake na mengineyo, na baada ya—ni kule kuja kwa Bwana na kufanywa upya kwa dunia.

¹⁵⁸ Nanyi mwaona, kulifanya hakika sasa, kuwa si- . . . Lakini jinsi Roho Mtakatifu alivyoliandika kwa nabii huyu, Yeye alisema, “Yeye ataigeuza mioyo ya baba, kwanza, iwaelekee watoto.” Ona? Huko kulikuwa kule kuja kwa kwanza kwa Yohana. Yeye aligeuza mioyo ya baba, wale wazee wetu wa kale, kuelekea ule Ujumbe wa watoto, ambacho kilikuwa kizazi kipya wakati ule, Yesu, katika kizazi hicho. Ndipo *na*, kiunganisho, kinafunanisha pamoja mioyo ya watoto iwarudie baba zao, ambayo maana yake ni kwamba, Ujumbe wa siku hizi utageuza mioyo ya watoto katika wakati wa kanisa ielekee kwenye imani asili ya Kipentekoste ya mwanzoni.

¹⁵⁹ Kwa hivyo itakuwa wawili mbalimbali—mjumbe mmoja, lakini inatofautisha pale kule—kule kuja kwa kwanza na kule kuja kwa pili kwa Yohana—au yule mjumbe, Eliya.

Mume wangu na mwanangu mdogo hawaamini . . .

Naam, nilijibu hilo. Najua nililijibu, kwa sababu mtu yule aliyeandika jina lake mle. Nakumbuka niliongea nao baadaye kuhusu hilo.

425. Twawezeje kupata mapenzi ya Bwana? Nyumbani mwetu—mwetu—Yatupasa tuhamie Jeffersonville, Indiana? Je, mtu aweza kuwa Mkristo na asiwapende watu we—weusi? Je, si Mungu anataka watendewe kama sisi, kwa sababu wana rangi nyeusi? Je, unge—wasemaje katika jambo hili? Je, unaamini katika utangamano au kubaguliaana?

¹⁶⁰ Naamini katika utangamano. Naamini kuwa mtu... Haidhuru ni wa rangi gani au yeye yu nani, yeye ni mtu kama tu nilivyo mimi. Naam hasa. Nami naamini, kama wangewaacha tu wale watu weusi, na hao wakomunisti hawangeingia kule na kuwashawishi. . .

¹⁶¹ Sasa, wao walitaka. . . Sasa, watu weusi halisi, kuna kundi halisi la wale waliozaliwa mara ya pili, watakatifu wacha Mungu kati ya watu hao. Naam, hakika. Kwa sababu tu ngozi yangu ni nyeupe na yao nyeusi, hilo halimaanishi lo lote kwangu. Yeye yu ndugu yangu kama yeye yuko katika Kristo.

¹⁶² Hiyo ndiyo sababu natofautiana na ujumbe wa Makaburu; hata hawaamini watu wale wana nafsi. Hilo ndilo lilinifanya nichukizwe kule. Nilisema, "Mtu huyo ni mtu kama nilivyo mimi. Yeye ana haki ya mambo niliyo nayo mimi. Ngozi yake haijalishi kamwe kwangu, au kwa ye yote aliyezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu."

¹⁶³ Bali nilisema, "Laiti wangaliwaacha hao watu weusi peke yao, hawangalisukumizwa." Nami nitasema hivyo toka katika mimbara hii. . . Tuna watu weusi wengi wajao hapa. (Sidhani kunaye ye yote humu usiku huu.) Lakini tuna watu weusi wengi sana wanaokuja humu kanisani; na ndugu, wamekaribishwa kama mtu mwingine ye yote alivyo. Wao ni Ndugu na dada zangu.

¹⁶⁴ Na baadhi ya watu wazuri sana niliowahi kukutana nao maishani mwangu ni baadhi ya hao watu weusi. Ndipo kunao wengine wao ambao ni wakaidi, vivyo hivyo tu kama watu weupe, au watu wa manjano, au watu wa rangi ya hudhurungi. Naam, hakika.

¹⁶⁵ Sasa, siamini katika ndoa baina ya watu wa rangi mbalimbali. Naamini kuwa mwanamume mweupe hapaswi kumwoa msichana mweusi, au msichana mweusi kuolewa na mwanamume mweupe, au wa manjano amwoe mweusi, au mweupe, au. . . naamini wa rangi hudhurungi, weusi, weupe, na rangi za watu ni kama maua ya bustani ya Mungu, nami siamini yapasa wachanganyishwe katika ndoa. Naamini hivyo ndivyo Mungu alivyowaumba, nami naamini hivyo ndivyo iwabidivyo kudumu.

¹⁶⁶ Nini... Lanipumbaza mimi kuwa nimeona msichana mweusi, mrembo mno, mtoto wa kupendeza, mrembo tu kama mwanamke ye yote ambaye ungetaka kumwona. . . Kwa nini anataka kuolewa na mwanamume mweupe kisha apate watoto

chotara? Msichana mweusi mwenye busara angetakia nini kitu kama hicho? Ni kwa sababu kitu fulani . . . huo ukomunisti . . . Na ingekuwaje mwa—mwanamume mweusi m—m—mzuri angetaka kumwoa mwanamke mweupe kisha amzalie watoto chotara?

¹⁶⁷ Siamini ni . . . naamini yapasa tu ukae jinsi ulivyo. Si—sisi ni watumishi wa Kristo. Na Mungu aliniumba . . . Kama Yeye aliniumba mimi, rangi yangu nyeusi, ningefurahia kuwa mtu mweusi kwa Mungu. Kama Yeye aliniumba wa manjano, ningefurahia kuwa mtu wa manjano kwa Kristo. Kama Yeye aliniumba mweupe, ninge- . . . ? . . . furahia kuwa mtu mweupe wa Kristo. Kama Yeye aliniumba wa rangi ya hudhurungi, au mwekundu, Mhindi, cho chote kile, ningebaki rangi ile ile yangu. Huyu ni mimi. Nataka kuwa jinsi Muumba wangu alivyoniumba.

¹⁶⁸ Kule chini siku hiyo katika Shreveport wakati ghasia hizo zilizuka, nao—na kulikuweco hao vijana wote weusi walioshawishiwa nje kule, ukomunisti . . .

¹⁶⁹ Niliwaambia ninyi hapa mimbarani, Martin Luther King ndiye mtu mwenye kuwiwa sana na watu weusi waliyewahi kuwa naye. Hiyo ni kweli. Mtu huyo ataongoza ma—maelfu yao katika mauaji (naam), ameshawishiwa na ukomunisti.

¹⁷⁰ Hebu nithibitishe ninayosema. Nilisema hayo yapata miaka miwili iliyopita. Tazama kile kinachotendeka hivi sasa. Wao walisema walikuwa wakipigania utangamano na hiyo sheria ilipowapa utangamano . . . Na kwenu watu msioamini katika kuchangamana, hamna haya. Taifa letu linaruhusu utangamano, nasi inatupasa kufanya yale bwana mkubwa anayosema yafanywe. Naam hasa.

Na sasa, mwasema . . . Msije mahali, na mengineyo hivyo, au kununua bidhaa, au kuketi nyuma ya gari kubwa la abiria, na mengineyo, la, bwana! Sheria inasema tu wao ni sawa kama tulivyo sisi, kwa hivyo sisi tu sawa kama wao walivyo; kwa hivyo na tutende hivyo. Hebu na tuwe hivyo. Na hivyo ndivyo hasa vile watu wote waaminio na waliozaliwa mara ya pili huamini. Na sasa, naamini hilo liko miyoni mwao.

¹⁷¹ Sijawahi kuwasikitikia watu kama ninavyowasikitikia hao maskini watu wa Afrika, jinsi wanavyotendewa. Na siamini upuzi huo. Mimi ni mtu wa Kusini; nilizaliwa ng'ambo ya mtoni kule, lakini mimi ni kama Abraham Lincoln; nilikuja hapa, kwa sababu naamini kuwa watu walizaliwa wakiwa sawa. Naam. Na siamini katika kuwabagua watu na mambo kama hayo, wakati watu hao . . . wamebatizwa na Roho Mtakatifu na kadhalika.

¹⁷² Lakini tazama, si wale watu weusi walio Wakristo halisi na wa kweli waliozaliwa mara ya pili wanaozusha mzozo huu wote. Mnataka kuwalaumu kwa hilo, vipi watoto wetu weupe walio wakaidi? Ona? Sasa, yafaayo bata Bukini wa kike yamfaa bata dume pia. Naam, watoto wetu weupe husababisha ghasia mara mbili zaidi ya zile hawa wamezusha. Hiyo ni kweli hasa. Iko

wapi? Katika vyuo vyetu vyote na kwingineko hivyo. Baadhi ya watu wetu wenye elimu ya juu sana wanazusha mambo hayo. Ona?

¹⁷³ Vema, ni nini? Sasa, kuwaonyesha ninyi kuwa hayo ni ukomunisti na si watu weusi hao, hivyo ndivyo ukomunisti umeingia kila mara ukatawale. Wanafanya hayo katika kila taifa. Hivyo ndivyo wafanyavyo, kuwafanya mpigane ninyi kwa ninyi, mapinduzi, ndipo wanaitwaa bila kufyatua risasi. Hawataki kulipua nchi hii; wanaitaka. Wanaweza kujipenyeza kisiri. Na sasa, wamepata nafasi ya kufanya hivyo, na wanajua jinsi mapinduzi ya kale yalivyokuwa, wakafikiri wanaweza kuanzisha uasi mwingine.

¹⁷⁴ Kuthibitisha ninayosema, baada ya wao kupata utangamano (wanao sasa, kisheria, halali), wanazusha mzozo mwingi sana sasa kuliko walivyofanya hapo mwanzoni. Ona? Yaonyesha kuwa ni ukomunisti na si nafsi hizo nzuri zilizozaliwa na Roho wa Mungu.

426. Je, tuendelee kuwa moto na kuhubiri Injili, au wakati umekwisha?

¹⁷⁵ La, endelea kuhubiri kwa nguvu uwezavyo kuhubiri. Ndugu, dumisha hilo; nakuunga mkono.

427. Ndugu Branham, ulipotoa unabii kuhusu: kutokula mayai, kutokuishi bondeni, unabii huo ulikuwa tu kwa ajili yako au ya kusanyiko? Vema.

¹⁷⁶ Miaka mingi iliyopita, yapata miaka thelathini iliyopita, nilitoa unabii kwamba itakuwa ya kwamba katika siku za mwisho kungetokea magonjwa kati ya wanyama, kati ya ng'ombe, na mayai, hata kwa mayai. Na itakuwa ya kwamba, kutakuweko na mayai ambayo hayafai kuliwa. Pia, itakuwa ya kwamba watu wanaoishi mabondeni... Sasa kumbukeni, nilitabiri hayo nyuma kule miaka thelathini iliyopita, ya kuwa itakuwa ya kwamba watu wanaoishi mabondeni, ya kwamba ningewauliza Wakristo waondoke mabondeni, na ya kwamba hawapaswi kula... Nyama mbalimbali na mambo kama hayo, yangekuwa sumu. Ingekuwa hatari (naamini jinsi nilivyosema) kwa watu kuishi mabondeni.

¹⁷⁷ Sasa, hilo lilikuwa kabla wao kuwa na yale mabaki au kujua lo lote kuhusu mabaki ya makombora. Lakini huyo alikuwa Roho Mtakatifu akinionya mimi. Na hivi sasa, hata kwa ng'ombe zetu (mnazona hazikubaliki sokoni) kunyunyuziwa kwao dawa ya D.D.T. kumezusha kitu fulani ndani ya ng'ombe hao.

¹⁷⁸ Tazama tena, huu upuzi wote wa kuchanganyisha mbegu na mengineyo wanayofanya yanaozesha kabisa jamii ya wanadamu wote. "Asilimia thelathini"—asilimia ishirini au thelathini, gazeti la Reader's Digest lilisema, "ya wagonjwa hospitalini wanawekwa ndani mle kwa ajili ya madaktari." Watakupe

dawa ya kuondoa hiki ndani yako, na yanaanzisha kitu kingine juu hapa.

¹⁷⁹ Na ulichunguza mayai? Mwaka uliopita watu wengi katika Louisville na Jeffersonville waliugua na kupelekwa hospitalini kwa kutapika kwa kula mayai ambayo kuku katika bonde hili hapa. . . Mayai ya bondeni yameambukizwa na yale mabaki. Na makwekwe ya sumu, na kadhalika, kila kitu kimeambukizwa.

¹⁸⁰ Lakini hapa ndipo unapolipata, Ndugu yangu. Naamini kwa moyo wangu wote kuwa imeandikwa katika Maandiko kwamba—kwamba hakuna chakula kinachopaswa kupokewa bila kushukuru, maana kimetakaswa kwa Neno la Mungu na kwa maombi. Ona? Ukikila, sema, “Bwana Yesu, Wewe ulinitayarishia mimi chakula hiki. Sasa, kwa imani takasa chakula hiki kwa ajili ya nguvu za miili yetu.” Ndipo ukile, kwa kuwa kila tufanyalo ni kwa imani.

Mpendwa Ndugu Branham, sababu za kutaliki mume mlevi?

¹⁸¹ Si—sipendi kuongea kuhusu hiyo talaka. Hiyo—hiyo. . . Ina—ni—ni—nitaongea kuhusu hayo baadaye.

428. Ndugu Branham, Ndugu (Ngoja kidogo. Linahusu mmoja wa wahudumu hapa. Hebu nilisome kwanza. [Ndugu Branham ajisomea mwenyewe swali hili—Mh.] Ngoja kidogo. Vema, nitawaambieni. Nitalisoma haidhuru.)—**Ndugu Branham, Ndugu Neville aliniambia kupitia kwa unabii ya kwamba BWANA ASEMA HIVI kwamba ningempokea Roho Mtakatifu. Akinambia na hakikisho hili kwamba ningempokea Roho Mtakatifu, bado sijampokea Roho Mtakatifu. Je, niendelea. . .**

¹⁸² Naam, hakika! Fanya hivyo. Endelea kuamini.

Tazama, simu—nilikuwa nimesimama kwa Ndugu Wood jana wakati simu ilipokuja toka kwa mwanamume fulani aliye katika kiti cha kusukumia wagonjwa, aliyekuwa hapa akiwa na mzigo kwa ajili ya ndugu au mtu fulani ambaye alikuwa—ambaye alikuwa mlevi na alikuwa amepitia kwa Chama cha Kuwasaidia Walevi wasinywe na akapigwa sindano, hospitalini, na kadhalika, na Ndugu Neville, akinena kwa lugha au kwa njia fulani alitoa u—unabii kuwa kitu fulani ingetendeka kwa manufaa ya mtu huyo katika siku chache zijazo au kitu kama hicho. Na mtu yule alipiga simu na kusema kuwa mtu huyu, kwa siku sitini na nane sasa, ametoka hospitalini, hajanywa pombe hata kidogo, wala kutafuna kibonge kimoja cha kumzuia asinywe, wala cho chote. Na jambo lile Ndugu Neville alisema katika unabii likatimia. Bwana asifiwe! Tunamwamini ndugu yetu kuwa mtu wa Mungu.

Mpendwa Ndugu Branham, je hayo. . .

¹⁸³ Sasa ngoja, hebu nikomee hapo kidogo. Sasa, hilo ndilo ninalojaribu kuwaambia watu. Ndugu Neville anaamini Ujumbe ule ule ninaomini. Ndugu Capps, Ndugu Beeler, Ndugu Ruddell, na ndugu hawa wote hapa wanaamini Ujumbe ule ule ninaoamini; wanauhumbiri, vivyo hivyo nifanyavyo.

¹⁸⁴ Na kama ukitaka, unataka kufanya hivyo kweli, utahama, na utastaafu au kitu kama hicho, na unataka kuja kwa ajili ya Neno, njoo hapa. Njoo hapa maskanini, hapo ndipo utakapolisikia.

¹⁸⁵ Hawa ni watu wacha Mungu. Ni watu walio na Roho Mtakatifu yule yule niliye naye—na mliye naye, hufundisha toka kwa Biblia ile ile na Ujumbe ule ule.

Mpendwa Ndugu Branham, je, wale watakaonena kwa lugha ni wale waliosalia . . .

Naam, nilijibu hilo. Enhee, nilijibu hilo. Mwanamke kunena kwa lugha.

Ndugu Branham, mahubiri yako ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, ni ubatizo kwa Jina la Yesu . . .

Naam. nilijibu hilo. Hebu tuone.

429. Ndugu Branham, Biblia inatwambia sisi kuwa m—mke apaswa kumtii mumewe. Mimi ni Mkristo na mume wangu ni mwenye dhambi. Yeye hunitesa katika kila njia awezayo, na kunikaza mimi kuenda kanisani, na kusoma Biblia yangu, kukana Neno. Nifanyeje?

¹⁸⁶ Ufanyeje? Sasa, sikia, inakubidi kumtii mumeo; hilo ni Neno. Sasa, akikwambia na kukukataza wewe kusoma Biblia, kuenda kanisani, au kitu fulani kama hicho, haikupasi kutii hayo, kwa sababu, “Yeye atakaye—asiyeacha baba yake, mama, mume, mke, au ye yote yule na kunifuata Mimi, hanistahili Mimi.” Sivyoye?

¹⁸⁷ La, usi . . . Wanaume wanapaswa—usi . . . Mwanamume hapaswi kutumia mamlaka hayo juu ya mwanamke eti kwa sababu tu yeye ni mtawala wake. Mungu ni mtawala wake juu yako, Ndugu. Ona? Na kama mke wako anafanya kitu kibaya, basi usi—basi una haki kumwambia, naye anapaswa kukusikia. Lakini huna haki yo yote ya kumchapa, au kumkokota hapa na pale, au—au kufanya mambo hayo. La, bwana!

¹⁸⁸ Waona, Mungu alimuambia mwanamume msaidizi, si zulia ya mlangoni. Kumbuka, yeye—yeye alikuwa mpenzi wako; anapaswa kuwa hivyo kila mara.

430. Lini na wapi ambapo watu wa Mungu watakusanyika kwa ajili ya Neno la mwisho?

¹⁸⁹ Katika Kristo. Naam! Kwa siku ya mwisho, watakusanyika katika Kristo. Msisahau hilo sasa. Tuna mahali pa kukutanikia; tunapo bila shaka.

431. Tunaitwa . . . (Sasa, hapa kuna swali hilo la juzi.) Tunaitwa ndege wachafu, kwa sababu tunaenda kwa kanisa la Junior Jackson. Wakati mwingine kwa sababu sisi tuko na— . . . Yeye hazingatii taratibu mpya za kanisa hapa kanisani. Je, tuko nje ya mapenzi makamilifu ya Mungu kwenda kule wakati mwingine?

¹⁹⁰ La, bwana! Naamini Junior Jackson kuwa mtu wa Mungu. Nimekwisha eleza hilo. Naamini . . .

¹⁹¹ Sasa, hatukubaliani kwa taratibu za kanisa. Sasa, naamini kuwa Junior—Junior . . . Sababu ya . . . Wangapi wanamjua Junior Jackson? Naam, twamjua huyo kuwa mtu mcha Mungu. Yeye anaamii Ujumbe huu vivyo hivyo kama nifanyavyo mimi, naye anaamini mambo haya. Kusema kweli, Junior na mimi ni marafiki mno, kama tu watu hawa wengineo, J.T. na—na Ndugu Ruddell, na Ndugu Jackson, na Ndugu Beeler, na ndugu hawa wengineo, sisi tu pamoja. Sasa, hatu—huenda tusione sawa jicho kwa jicho (ona?), lakini tunaamini Ujumbe uu huu (ona?), nasi tunaungana. Pale kuna Ndugu Hume kule pia, mmishenari, na lo, wengine wengi mbalimbali, ni . . . Wakati mwingine hata siwezi kutaja majina yao, lakini una—unajua nakusudia wewe haidhuru, Ndugu. Hakika.

Ungetaka kuacha kufanya kazi ya uuguzi . . .

¹⁹² Niliuliza hilo. Mwakumbuka? Ni dada mpendwa aliyetaka kujua kuhusu kufanya kazi ya uuguzi.

Nilipokuwa mdogo—nilimwambia kila mtu kuwa nilitaka kuwa mhubiri. (Nilijibu hilo. Nilijibu hilo pia.) Basi afanyaje sasa?

¹⁹³ Vema, hii ni barua toka kwa m—mhudumu mfanyi kazi wa Kristo, ambaye si . . . Ni barua tu ya kibinafsi kwangu. Inatoka kwa Ndugu Pat Tyler, mojawapo wa ndugu zetu hapa kanisani.

Yote yamekwisha. Namshukuru Bwana. Nina shukrani kwenu watu. Napata tu . . . [Sehemu yake haipo kwenye kanda—Mh.]

. . . tu moja

Faraja yetu na ulinzi wetu.

¹⁹⁴ Nashangaa kama Dada Wilson bado yuko jengoni? Nilimwona hapa. Mwajua yale niliyokuwa nikifanya muda mchache uliopita, Dada Wilson? Nilikuwa nikizitazama zile picha tulipoweka lile jiwe la pembeni. Nilitazama ile picha na kujiona mimi pamoja na Hope kabla hatujaoana. Hata sikujua kwamba . . . Nakumbuka nilipoona picha fulani nilipotoka kwa moja ya mapigano yangu, niliposhinda ubingwa. Nilitazama picha yangu usiku uliopita nilipokuwa mlinzi wa hifadhi za wanyama hapa Indiana. Nami nawaza kuhusu kanisa hili. Mwajua, nadhani hukuna ila kama mtu mmoja pekee anayeketi hapa usiku huu toka kwa kundi hilo aliyesalia. Wangapi

wako hapa tangu tulipoweka lile jiwe la pembeni nyuma kule mwanzoni, inueni mikono yenu.

¹⁹⁵ Ndugu yangu, Dada Wilson, nawatakeni ninyi—kuwaulizeni mambo fulani mawili. Mwakumbuka jinsi sisi sote tulivyoanza? Mwakumbuka ile sakafu ya kale ilipokuwa imejawa matope? Tulikuwa na madirisha makuukuu yaliyotikisika. Tulikuwa na senti themanini kuyaanzishia. Tita kubwa la magugu, haya yote yalikuwa kama msitu nyuma yetu hapa tulipoyajenga, maskani haya.

¹⁹⁶ Tutazameni sisi sote tulioweka nadhiri yetu na kutembea kuzunguka madhabahu. Tumewaona wakija na kuondoka, mmoja kwa mwingine. Mmetambua wale waliokaa na Ujumbe, jinsi walivyoenda? Sasa, waza kuhusu wale walioacha Ujumbe, jinsi walivyoenda. Wazia hilo.

¹⁹⁷ Tuko hapa usiku huu, baada ya kundi hilo lote la mara tatu ya tulio nao hapa sasa kwa mikutano yetu iliyojaa sana. Wazia hilo, wakati mabasi ya shule yangepakiwa hapa kutoka kila mahali nchini humu, huku na huko kwa kundi hili. Hata waliosalia wakiwa kwenye mahema walimoketi mle kuwashughulikia, na bado hata hungewaketisha watu po pote, kuwakusanya pamoja. Nilikuwa tu mhubiri kijana. Ona? Na kati ya hao maelfu tuliokuwa nao, ni watatu wetu waliobakia ndani humu usiku huu.

¹⁹⁸ Namkumbuka Dada Wilson pale nilipoitwa kwake kando ya kitanda akifa kwa ugonjwa wa Kifua kikuu, akitokwa na damu hata shuka na mifuko ya mto zilikuwa pale, zimelowa damu. Nakumbuka Roho Mtakatifu akikomesha damu ile. Siku chache baadaye nilimbatiza katika Mto Ohio katika maji yenye barafu katika Jina la Yesu Kristo, na kumketisha nyuma ya motokaa yangu wazi, motokaa yangu wazi, motokaa ndogo, na kuiendesha toka Utica . . . Sivyo? Toka . . . [Dada Wilson aongea na. Ndugu Branham—Mh.] Naam! Dada Hope, mke wangu, Dada hapa, walikuwa katika kiti cha mbele cha ile motokaa ndogo ya roadster, na mama mkwe yangu na Dada Snelling nyuma. Nina picha yao. Dada Snelling, Mama, hao wote, Bi. Weber, Bi—mama mkwe wangu, sisi sote chini kule, na Meda, msichana mdogo tu amesimama pale, na sasa, ni mwanamke mwenye mvi [Dada fulani aongea na Ndugu Branham—Mh.]

¹⁹⁹ Nakumbuka ile siku ya vijikaratasi vya kubandikia kupata pesa zetu za kwanza. Nami nakumbuka Hope akisimama pale pembeni. Yeye alikuwa tu msichana, mwenye umri wa kama miaka kumi na sita hivi; yeye alikuwa akiuza hivi, akishikilia hivyo vijikaratasi vya kubandikia. . . . Akiwapa karatasi hiyo. . . . Yeye ange ingiza ndani. . . .

Mlevi alikuja akitembea barabarani; naye kasema, “Kunradhi, Binti!” Kasema, “Unauza nini?”

Kasema, “Si kitu. Kwa hivyo nakupa kijikaratasi hiki cha kubandika.” Kasema, “Ni mchango kwa ajili ya kanisa. Ukitaka kuweka cho chote ndani humu kwa ajili ya mchango, tunajaribu kupata pesa za kutosha kujenga maskani kwa ajili—katika mji huu.” Kasema, “Ukitaka kuweka ndani humu cho chote, waweza, lakini kama . . .”

Kasema, “Sina kitu.”

Kasema, “Chukua kijikaratasi hiki haidhuru.” Yeye alikichukua na kukitazama. Upande mmoja kasema—kasema—kasema, “Utaishi wapi Milele?” Na upande wa pili ulikuwa na alama ya kuuliza. “Utakaa wapi utukufuni? Swali.”

Yeye akayumbayumba nyuma akakitazama; naye kasema, “Binti, unauliza swali gumu!”

Yeye kasema, “Lakini halina budi kutatuliwa!” Na hiyo ni kweli. Yeye amevuka pazia zile usiku huu. Nakumbuka maneno ya mwisho aliyosema. Nakumbuka yale niliyomwambia; nayakumbuka. Naam, bwana!

²⁰⁰ Maji mengi yaisha pita mtoni. Tulikuwa tunasimama kule—na hata kabla hatujapata kanisa, tulikuwa tukisimama na kushikana mikono na kuimba wimbo huu hapa. Naweza tu kuusikia. Myrtle alikuwa tu mtoto mdogo wakati huo. Nina picha ya maskini Leroy akisimama nje pale, ni kama kitoto kidogo.

Kibarikiwe kifungo
Kinachotunganisha mioyo,
Ushirika wetu wa fikira zetu
Ni kama ule wa mbingu.

²⁰¹ Tunapoimba huo kunao wengi mno wanaongoja kule ng’ambo kwa ajili ya kuja Kwake.

. . . Nyikapo,
Hiyo yatufadhaisha; (Mnapendana hivyo?)
Bali tungali pamoja rohoni,
Na kutumainia kukutana tena.

²⁰² Ndugu Freeman, umekaribia kule, sivyo? Nilikuwa tu nikiwazia, nilijua tulipoenda kwa Ndugu Roy. Mwakumbuka jamaa ya Adcocks? Nilikutana na Kenneth. Jina la dada yake lilikuwa nani? [Ndugu Freeman aongea na Ndugu Branham—Mh.] Nina picha yao; sisi sote tulikuwa tumesimama nje pale huku tumekumbatiana, kuzunguka upande wa mbele, Dk. Roy E. Davis, mchungaji. Nilikuwa nikizitazama muda mchache uliopita. Doc alizileta hizo picha za kale hapa. Zilinifanya nijisikie kiajabu sana humu. Sasa hilo—wengi wao wameondoka (ona?)—wameaga dunia. Haitachukua muda mrefu hata nasi tuondoke. Ona? Lakini . . .

Tutawanyikapo,
 Hiyo yatufadhaisha;
 Bali tungali pamoja rohoni
 Na kutumainia kukutana tena.

²⁰³ Mwakumbuka Ndugu Bosworth? Kabla tu kuvuka kwake, yeye aliamka mle chumbani akatembea kote sakafuni, akasalimiana na baba yake, na mama, na wale waongofu aliowaleta kwa Kristo. Miaka arobaini, hao walikuwa tayari wamekufa kwa miaka arobaini au hamsini. Yeye aliwaona wamesimama mle chumbani, wakijaribu kufanya kila mtu awaone. Ilikuwa nini? Mzee yule alikuwa akivuka kuingia nchi hiyo niliyokuwamo katika ono asubuhi hiyo. Hiyo ni kweli.

²⁰⁴ Niliwaona ng'ambo kule; walikuwa vijana tena. Sisi bado tumeunganika katika mioyo; tunatumainia kukutana tena. Naam, Mungu awabariki.

²⁰⁵ Nilitazama mle jengoni nikiongea kuhusu rafiki zangu weusi, nami namwona Ndugu na Dada Nash wameketi nyuma kule. Sikujua mlikuwa pale. Nilitazama tu nyuma; wako nyuma kule. Na Ndugu huyu mwingine anayeketi hapa. . . Je, huyo ni Ndugu yule anayenishangilia kwa shangwe kuu mno nyuma kule mara kwa mara, anayeketi upande huu? Nimesahau jina lake. Ndugu Wood alisema yeye alikuwa akiongea naye. Yeye alisema, "Wajuaje? Roho anigusapo, sina budi kupiga shangwe 'Heii!'" Kasema, "Natumai simuudhi ye yote." Usipopiga shangwe "Heii!" yaniudhi mimi. Mungu akubariki. Nawapenda ninyi Ndugu, Dada. Naam.

²⁰⁶ Ndugu Nash, Dada Nash, mwajua nawapenda. Naam, bwana! Ninyi ni ndugu zangu na dada katika Kristo Yesu.

²⁰⁷ Marafiki wapendwa, wengine wengi, kama nimewakosa wengine wao, milango hiyo i wazi hapa kwa ajili yenu. Milango ya Mbinguni pia itafunguliwa pia.

Bali tungali pamoja rohoni
 Na kutumainia kukutana tena.

Ye—Yesu Kwa Imani, sasa, tunapoimba. Hebu na tuimbe tena sasa. Ni wakati wa kuenda nyumbani sasa.

Yesu kwa imani
 Nakutumaini,
 Peke yako;
 Nisikie sasa,
 Na kunitakasa,
 Ni wako kabisa
 Tangu leo.

Hebu tujaribu huo *Mtakatifu, Mtakatifu* tena, sivyo? Tupe sauti kwa kinanda, Dada. Mwaujua? Mwakumbuka wakati Dada Gertie na wengineo walipokuwa wakiuimba?

208 Siku inafifia magharibi, Mbingu zaibariki nchi—nchi imebarikiwa. Jinsi nipendavyo machweo ya jua la jioni linapotua, ndege wakitoa wito wao wa mwisho. Hilo lapasa kumjia kila mmoja wetu basi. Nafikiri ya kwamba wakati wa jioni... Je, mlitambua, upepo utakoma kuvuma; ndege watanyamaza. Ona? Ni nchi inayokufa, siku inakufa ikazaliwe tena kesho asubuhi. Vema sasa. Hebu tuujaribu sasa tukiweza.

Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu uliye juu.

Njoo hapa kidogo. Na—na—na ya kwamba si—sidhani naujua kwa sauti hiyo. Hebu niujaribu bila hiyo sauti ya kinanda. Ona? Hebu tuone kama tunaweza kuuimba. Sasa, najua—huenda nikakosea kwa sauti. Ona? Ninyi mnisaidie sasa, kila mmoja wenu, sasa.

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana
Mungu uliye—majeshi!

Mbingu na nchi vimejawa Nawe:

Mbingu na nchi zinakusifu,

Ee, Bwana uliye juu sasa! (Mwaupenda huo?

Je, hilo halitendi jambo fulani kwenu? Hebu
tuujaribu tena!)

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana
Mungu uliye juu!

Mbingu na nchi vimejawa Nawe;

Mbingu na nchi zinakusifu,

Ee, Bwana uliye juu sana!

209 Naupenda huo, nanyi je? Ee, napenda hizo nyimbo nzuri za kale. Kuna kitu fulani kuhusu hizo nyimbo ninachokipenda. Mwaweza kuwa na maskini nyimbo zenu zote zilizokatakatwa mtakazo. Nipe mimi hizo; nazipenda hizo. *Pita Pazia Iliyopasuliwa*, nyimbo hizi zingine zote tamu hivyo; napenda nyimbo hizo. Nafikiri kuimba ni sehemu ya ibada (naam, bwana!), kumwambia Bwana sifa.

210 Vema, wa kumalizia kwetu sasa—wimbo, ni *Peleka Jina La Yesu*. Na Bwana awabariki ninyi sasa tunaposimama.

Peleka Jina la Yesu
Ko kote uendako;
Litafurahisha moyo,
Peleka uendako

Thamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, na tamu,
Ni Jina Lake Yesu.

Sasa hiki ndicho kifungu ninachokipenda, na ni onyo kwenu sasa. Ufanyeje?

Peleka Jina La Yesu
Liwe silaha zako; (sikiza!)
Utakapojaribiwa, (Ufanyeje?)
Lilia Jina hilo.

Thamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, na tamu,
Ni Jina Lake Yesu.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa.

Hata twonane huko juu,
Hata twonane Kwake kwema; (Kwake
kwema)
Hata twonane huko juu,
Mungu awe nanyi daima . . .



Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org